

**WASAUDIA HAWAJAKATA TAMAA KUMSAJILI MBAPPE**

UKURASA 21


# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumatatu Desemba 18, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581528

nipasheTZ nipasheTZ

0745 700710 LIKE & FOLLOW US The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com


# Siku 13 moto kwa ma-DED



• **Madiwani** wakwaa kashfa nzito; Samia apiga simu, aahidi neema kwa walimu... *Endelea ukurasa 2&7*



Baadhi ya wafanyabiashara wakiuza vyakula na bidhaa zingine katika Stendi Kuu ya Mabasi Moshi wiki iliyopita. **PICHA: MARY MOSHA**

RIPOTI MAALUM -2

## Madaktari bingwa waipa angalizo serikali vyakula vya stendi

UKURASA 4

UKURASA WA 3

**Waziri** asema Rais amefanikiwa katika kuimarisha uhusiano kimataifa

UKURASA WA 3

**Aliyehukumiwa** miaka 30 gerezani, akata rufani, afungwa maisha




UKURASA WA 17

**SMZ** yazifunga zahanati tano ilizobaini shida

# Milioni moja wachaguliwa kujiunga sekondari mwakani

• **Wamo** 1,400 wa mkondo wa amali za uhandisi... *Uk. 2*

**MICHEZO** **GAMONDI ALIA STRAIKA WAKIISUBIRI MEDEAMA** UK.24 **KATUNI** UK.6




Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, akiwasalimia mama na baba lishe walayani Kigamboni baada ya kuwakabidhi majiko ya gesi katika hafla ya kukabidhi vifaa vilivyotolewa na wadau kwa ajili ya makundi mbalimbali mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Siku 13 moto kwa ma-DED

## -Samia aahidi neema kwa walimu

**Na Augusta Njoji,** GEITA

ZIMEBAKI siku 13 kuumaliza mwaka huu, yaani Desemba 31, 2023, tarehe ambayo ni mwisho wa ukamilishaji ujenzi wa miundombinu ya elimu.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa ameendelea kubana wakurugenzi wa halmashauri kukamilika ili kupokea wanafunzi tarehe 8 ya mwezi ujao.

Ni ujenzi huo unaotekelezwa kupitia fedha za Mradi wa Uboreshaji Elimu ya Awali na Msingi (BOOST) na ule wa Uboreshaji Elimu ya Sekondari (SEQUIP).

Kwa nyakati tofauti akiwa katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo mkoani Geita wiki iliyopita, Waziri Mchengerwa alisema mkurugenzi wa halmashauri atakayeshindwa kukamilisha kwa muda uliopangwa ujenzi wa shule na madarasa, atapendekeza kwa Rais aondolewe kwenye nafasi yake.

"Nimewapa wakurugenzi kazi ya ujenzi wa madarasa mwaka mzima, tumewapa muda wa kutosha na maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan Desemba 31 madarasa yawe yamekamilika, ongezeni kasi mkamilishe, watu wajenge usiku na mchana.

"Madarasa yalipaswa kukamilika Septemba 30, 2023, lakini wengine wanajivutavuta na tamko hili alitoa aliyekuwa Waziri wa TAMISEMI wakati huo, Angellah Kairuki. Nilipoingia Septemba Mosi, mimi nikawaambia maelekezo yapo palepale na nikaona huruma nikaongeza muda hadi Desemba 31," alisema.

Waziri huyo alisema hataki kuona wanafunzi Januari wanakosa madarasa kwa sababu ya kutokamilisha ujenzi wake.

"Nendeni mkasimamie miradi, fedha zimetolewa, sitegemei kusikia kuna mkurugenzi ambaye ameshindwa kutekeleza miradi katika maeneo yake," alionya.

Waziri huyo alisema serikali imedhamiria kuweka usawa wa elimu kwa watoto wa kitanzania kwa kujenga miundombinu ya kisasa.

Alisema serikali imekuwa inatoa takribani Sh. bilioni 800 kwa mwaka, ili kuruhusu watoto wa kitanzania wasome bure kuanzia awali mpaka kidato cha sita, ikiwa ni katika kuweka uwiano wa usawa kwa kila Mtanzania bila kujali anaishi wapi huku viwango vya shule hizo vikiwa sawa.

"Tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kufua ndoto za Baba wa Taifa kwenda kumaliza ujinga maradhi na umaskini kupitia elimu," alisema.

Waziri huyo alisema ujenzi wa shule hizo pia unaondoa mfumo wa zamani hususani kwenye maeneo ya msongamano wa kuwafanya wanafunzi kusoma kwa zamani. "Kutokana na msongamano wa wanafunzi na uhaba wa miundombinu, wanafunzi walikuwa wanalazimika kusoma kwa zamu, wengine kuja asubuhi wengine kuja mchana. Sasa Rais Samia ameondosha ndoto ya wanafunzi kusoma kwa 'shift' (kupokezana)," alisema.

Aliagiza uongozi wa mkoa kuhakikisha unaongeza kasi ya uandikishaji, ili miundombinu hiyo itumiwe kwa lengo lililokusudiwa.

Awali, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Magogo, Juliana Kusigwa, alisema wamepokea Sh. milioni 609.3 ikiwa ni Sh. milioni 540.3 za mradi wa BOOST na Sh. milioni 68 kutoka halmashauri, zilizotumika kulipa fidia ya eneo na Sh. milioni moja kama nguvu za wananchi.

Alisema fedha hizo zimejenga kujenga shule mpya yenye madarasa mawili ya elimu ya awali na madarasa 14 ya msingi kwa mikondo miwili, matundu ya vyoo, jengo la utawala na kichomeataka.

Alieleza kuwa hatua hiyo imepunguza msongamano wa wanafunzi katika shule za Ngurzombili na Mwatulole na kuboresha mazingira ya kujifunzia na kupunguza utoro na wanafunzi kutembea umbali mrefu kufuata huduma ya elimu.

**SIMU YA SAMIA**

Katika hatua nyingine, Rais Samia amesema serikali inafanyia kazi suala la makazi na maslahi ya walimu nchini ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi.

Akizungumza jana kwa njia ya simu kupitia Waziri Mchengerwa kwenye mkutano wa walimu wa shule za serikali na binafsi nchini unaofanyika jijini Mwanza, Rais Samia alisema serikali ina imani kubwa na walimu kwa kuwa kundi hilo ni tumaini kubwa katika ujenzi wa nchi.

"Si mnajua sisi sote tulipita mikononi mwa walimu. Kwahiyo, nami nipo pamoja nanyi, pamoja na jitihada tunazochukua lakini bado tunaendelea kujipanga vyema ili kutimiza matakwa ya walimu. Ninajua moja ya maswali yanayowasumbua ni makazi," alisema.

Aliahidi kuwa kwa kuanzia, bajeti ya mwaka ujao (2024/25), serikali itajielekeza kujenga nyumba nyingi za walimu ili wapate utulivu katika kufanya kazi yao.

"Pamoja na makazi, ninatambua pia maslahi ya walimu, na lenyewe tunalifanyia kazi ili walimu mpate maslahi yetu kwa vyema na mfanye kazi ya kutufundishia watoto wetu ambao ndio watakuja kushika taifa hili baadaye," alisema.

Mkuu wa Nchi aliwataka walimu kumweleza Waziri Mchengerwa kero zao ili azifikishe kwake na kuahidi kuzifanyia kazi kwa pamoja.

Naye Waziri Mchengerwa alisema walimu wanamuunga mkono Rais Samia na wameandaa kapu na kuchangisha fedha, wako tayari kumchukulia fomu mwaka 2025 ili kumshukuru kwa kazi kubwa aliyofanya kwenye ujenzi wa miundombinu na upandishaji madaraja. Walikaa miaka saba hadi 10 pasipo kupandishwa vyeo na madaraja kazini.

UDAHILI KIDATO CHA KWANZA

# Milioni moja wachaguliwa kujiunga sekondari mwakani

**Na Augusta Njoji,** MWANZA

WANAFUNZI 1,092,984 waliofaulu mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi mwaka 2023, wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwakani huku 1,410 wakipangwa kwenye baadhi ya shule za sekondari za mkondo wa amali za kihandisi ikiwa ni kuanza utekelezaji wa mtaala mpya wa elimu.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, alisema kati ya idadi hiyo wasichana ni 585,051 na wavulana 507,933 wamefaulu na kupangiwa shule za sekondari za serikali ili waanze masomo ya Kidato cha Kwanza Januari, 2024.

Pia alisema idadi hiyo inajumuisha wanafunzi wenye mahitaji maalum 3,587 wakiwamo wasichana 1,590 na wavulana 1,997."Wanafunzi waliopangiwa shule 48 za bweni za kitaifa ni 5,606 sawa na asilimia 0.5, katika shule teule za mikoa ni 17,412 sawa na asilimia 1.6 na shule 4,566 za kutwa ni 1,069,966 sawa na asilimia 97.9," alisema.

Alifafanua waliochaguliwa shule za wenye ufaulu wa alama za juu ni 942 na watakwenda shule za sekondari saba ambazo ni Ilboru, Msalato, Kibaha, Kilakala, Mzumbe, Wavulana Tabora na Wasichana Tabora.

"Wanafunzi 1,410 wakiwamo wavulana 1,136 na wasichana 274 wamechaguliwa kujiunga katika shule za sekondari tisa za amali za kihandisi ambazo ni Bwiru Boys, Ifunda, Mwadui, Iyunga, Moshi, Mtwara, Musoma, Tanga na Chato. Idadi hii ya wanafunzi inajumuisha wenye mahitaji maalum 274 wakiwamo wasichana 31 na wavulana 243," alisema.

Mchengerwa alisema wanafunzi 3,254 wakiwamo wasichana 1,511 na wavulana 1,743 wamechaguliwa kujiunga katika shule za sekondari 32 za bweni za kitaifa za kawaida. Idadi hii inajumuisha wanafunzi wenye mahitaji maalum 1,629 wakiwamo wasichana 836 na wavulana 793, jumla ya wanafunzi 17,412 wakiwamo wasichana 7,816 na wavulana 9,596 wamechaguliwa kujiunga na shule za bweni teule na zile za wasichana za mikoa. Shule za wasichana za mikoa saba zimepangiwa wanafunzi wasichana 897 wakijumuishwa wanafunzi wenye mahitaji maalum 116.

Aidha, alisema shule zingine za bweni za wasichana za mikoa 19 zitapangiwa wanafunzi mwishoni mwa Desemba 2023 baada ya kukamilisha usajili wa shule hizo.

"Wanafunzi 1,066,966 wakiwamo wasichana 573,018 na wavulana 496,948 wamechaguliwa kujiunga katika shule za sekondari 4,566 za kutwa ambazo hupokea wanafunzi kutoka katika kata au eneo la karibu na shule ya msingi aliyosoma mwanafunzi husika. Idadi hii ya wanafunzi ni sawa na asilimia 97.89 ya wote waliofaulu na kupangiwa shule za sekondari za serikali," alisema.

Aliagiza shule za sekondari ambazo zimepangwa kutekeleza mkondo wa amali za kihandisi na zingine kutumia kipindi cha wiki sita kutoa maelekezo kwa wanafunzi ili kuchagua aina ya amali au mchepuo wanaopenda kusoma.

"Natoa wito kwa wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya, viongozi na watendaji wa halmashauri kwa kushirikiana na wadau wa elimu kuhakikisha wanafunzi wote waliochaguliwa wanaanza masomo yao mwezi Januari, 2024 bila vikwazo vya aina yoyote ili kutekeleza azma ya serikali ya utoaji wa elimu msingi bila ada," alisema.

Aliwaagiza wakuu wa mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kufanya maandalizi yote ikiwamo ujenzi wa miundombinu yote kwa ajili ya kupokea wanafunzi wa Kidato cha Kwanza mwaka 2024 inakamilika kwa wakati kama ilivyopangwa.

"Shule zote mpya za sekondari za kata na zile za wasichana za mikoa zinakamilishwa ujenzi wake na kusajiliwa ifikapo Desemba 30, 2023, shule za bweni za wasichana za mikoa zinawekewa bajeti ya chakula katika kipindi hiki cha marekebisho ya bajeti, wanafunzi wote waliochaguliwa na kupangiwa shule wahakikishe wanaripoti shuleni," alisema.

Aliwahimiza wazazi au walezi na jamii kushirikiana na uongozi wa wilaya, halmashauri na shule ili wanafunzi wote waliochaguliwa wanaandikishwa, wanahudhuria na kuendelea na masomo yao hadi watakapohitimu elimu ya sekondari.

Naibu Katibu Mkuu wa ofisi hiyo, Charles Msonde, alimhakikishia waziri kuwa maelekezo aliyoyatoa kwenye upangaji wanafunzi yamezingatiwa kwa kufuata uzalendo na uaminifu wa hali ya juu na kwa wanafunzi ambao hawajaingia kwenye mchakato wa shule pendwa wamepangwa kwenye shule za kutwa zilizo jirani na maeneo yao na wapo zaidi ya asilimia 97.

**HABARI KITAIFA**

# Serikali yaahidi ushirikiano kukabili ujangili nchini

**Na James Kandoya**

SERIKALI imeahidi kuendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo kuendeleza uhifadhi wa wanyamapori na kukomesha ujangili.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki, alisema hayo wakati wa uzinduzi wa Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Wanyamapori na Mpango wa Usimamizi wa Tembo Tanzania 2023-2033 uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Uzinduzi huo ulifanywa na wizara kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Matifa la Maendeleo (UNDP), Mfuko wa Mazingira Duniani (GEF) na wadau wengine wa maendeleo wanaojihusisha na uhifadhi wa wanyamapori.

Alisema serikali imeweka mikakati mbalimbali ya uhifadhi wa wanyamapori, na kwamba mbinu zinazotumika zitaongeza watalii kufikia zaidi ya bilioni tano mwaka 2025 na kuingiza kipato cha zaidi ya Dola za Marekani bilioni sita.

"Hatuwezi kuwa na utalii imara bila kuweka mkakati mzuri wa uhifadhi wa wanyamapori," alisema.

Alitoa wito kwa sekta binafsi na wadau wanajenga hoteli za kutosha ili watalii wapate sehemu nyingi za kulala.

Takwimu za hivi karibuni za wizara za 2022 zinaeleza kuwa tangu mwaka 2014 Tanzania imekuwa na ongezeko la tembo kutoka 43,330 hadi 60,000 na faru ikifikia zaidi ya 200.

Mwakilishi Mkazi wa UNDP, Shigeki Komatsubara, aliipongeza Tanzania, wadau wa utalii na wananchi kwa jitihada za kupambana na ujangili nchini.

Mradi wa IWT ni kichocheo cha mabadiliko chanya, yanayoonyesha umuhimu wa ushirikiano wa kimataifa katika kuhifadhi wanyamapori na kuongeza kuwa UNDP itaendelea kuisaidia Tanzania katika kuendeleza juhudi zake za kupambana na ujangili.

"UNDP inasimama pamoja serikali na washirika wake katika vita vya kupambana na ujangili na kulinda hazina ya Tanzania kwa vizazi vijavyo. Tutaendelea kusaidia nchi katika kuendeleza juhudi zake dhidi ya ujangili," alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha Mawakala wa Utalii Tanzania (TATO), Wilbard Chambulo, alisema sekta binafsi iko tayari kushirikiana na serikali kuhakikisha sera iliyozinduliwa inatekelezwa vizuri ili kukuza utalii nchini.

"Hadi sasa utalii wa Tanzania uko mbali sana hakuna nchi yoyote za jirani zinazoweza kutufikia kutokana na vivutio vyetu vya kipekee," alisema na kuongeza kuwa juhudi za pamoja zitasaidia kuongeza idadi ya watalii nchini.




Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Riziki Pembe Juma (kulia), akipokea cheti kutoka kwa vijana wa mtandao wa wanawake barani Afrika, ikiwa ni tuzo ya mafanikio ya maisha kwa niaba ya Rais wa Samia Suluhu Hassan, katika kongamano la vijana lililofanyika ukumbi wa Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Nyerere, Kibaha mkoani Pwani, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri asema Samia amefanikiwa kuimarisha uhusiano kidiplomasia

**Na Halfani Chusi**

WIZARA ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imesema Rais Samia Suluhu Hasasan amefanikiwa kuimarisha ushirikiano kati ya Tanzania na nchi jirani.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam kuhusu mafanikio ya ziara za Rais Samia na viongozi wengine wa serikali nje ya nchi, Waziri January Makamba alisema fursa nyingi za kiuchumi zimeendelea kufunguka kwa ajili ya nchi.

Alisema mbali na kuunganisha ushirikiano, ziara hizo pia zimeleta mafanikio katika nchi, ikiwamo kupanua masoko ya nje kwa bidhaa za ndani.

"Pia kuongeza kiwango na idadi ya watalii waliokuja nchini, kutafuta fedha za kugharamia maendeleo kwa ajili ya miradi ya kimkakati na kuimarisha amani na usalama kikanda," alisema.

Alizitaja faida zingine ni kupata fedha za ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) na Benki ya Maendeleo ya Kilimo kuongezewa mtaji ili kuwawezesha wakulima wengi zaidi nchini.

Alisema ziara ya India ilileta mafanikio katika sekta za kimkakati kama afya, viwanda na biashara, ulinzi na usalama, elimu, teknolojia ya habari na mawasiliano, uchumi wa buluu, maji na kilimo.

Kwa mujibu wa January, soko la tani 200,000 za mbaazi kwa kila mwaka na uanzishwaji wa Taasisi ya Teknolojia ya India nchini, kufanyika kwa kongamano la biashara na uwekezaji kati ya nchi hizo lililoazimia kuongeza soko la bidhaa za kilimo na kuongeza uhakika wa soko, ni matunda ya ziara hiyo ya Rais.

Alitaja faida nyingine kuwa ni kuongeza muda ambao kampuni za India zinaruhusiwa na Benki Kuu ya India kutoa bidhaa kwa mkopo kwa kampuni za Tanzania kutoka siku 180 mpaka 360, sekta binafsi kukubaliana kuongeza ushirikiano katika sekta za kilimo, teknolojia, sanaa na burudani, uwekezaji na biashara, ili kukuza uchumi wa nchi zote mbili, pamoja na baadhi ya kampuni kubwa kuonesha nia ya kuja kuwekeza.

Kuhusu ziara ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), January alisema ziara hiyo ilisaidia kuwezesha Tanzania kufuatilia kwa ukaribu na kushiriki kikamilifu katika juhudi za kutafuta amani ya kudumu huko Congo, ikizingatiwa ukaribu wa kijiografia na uhusiano wa kihistoria uliopo baina ya nchi hizo.

Waziri huyo alisema ziara hiyo ilichochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi, ikiwamo biashara na uwekezaji kufuatia kuwapo amani na usalama pamoja na uimarishaji ustawi wa jamii hususan katika maeneo ya mipakani kutokana na kuimarika kwa hali ya usalama.

"Mwezi uliopita Rais alishiriki kwenye mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28) uliofanyika Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).

"Mafanikio yaliyopatikana kutokana na ziara hiyo ni pamoja na kuzindua mradi wa matumizi ya nishati safi unaolenga kuwasaidia wanawake hususan wanaoishi vijijini.

"Tanzania na Umoja wa Falme za Kiarabu zilitia saini hati tatu za makubaliano ya ushirikiano katika maeneo ya elimu, teknolojia na diplomasia," alisema January.

Alisema ziara ya Marekani imeleta neema. Nchi hiyo imeahidi kujenga kiwanda kikubwa nchini cha kuchakata madini yanayotumika kutengeneza betri za magari ya umeme kwa ajili ya soko la Marekani na dunia kinachotarajiwa kukamilika mwaka 2026.

Alisema kiwanda hicho kinatarajiwa kuongeza mauzo ya Tanzania nje ya nchi na kuzalisha ajira kwa Watanzania, kutoa msaada wa nyongeza wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 1.3 kupitia Shirika lake la Misaada la (USAID) kwa ajili ya kukabiliana na magonjwa ya mlipuko.

# Kutoka kifungo miaka 30 jela hadi cha maisha

**Na Said Hamdani,** LINDI

MUSA Ulaya (45), aliyehukumiwa na Mahakama ya Wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi kifungo cha miaka 30 gerezani kwa kosa la kumwingilia kinyume cha maumbile kijana mwenye umri wa miaka 15, ameongezewa adhabu ya kifungo cha maisha.

Uamuzi huo umetolewa na Hakimu Mkazi Mwandamizi, Conslata Singano, baada ya kupitia rufani iliyowasilishwa katika mahakama hiyo.

Mei 14, mwaka huu, Musa alihukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani baada ya kukutwa na hatia ya kumwingilia kinyume na maumbile kijana huyo.

Kabla Hakimu Singano hajamwongezea adhabu hiyo, Mwanasheria wa Serikali, Irani Hamza alisimama na kuibua hoja kupitia kifungu cha 154, kifungu kidogo A, kanuni ya adhabu sura ya 16 rejeo 2022 na kueleza mfungwa Ulaya anastahili kutumikia kifungo cha maisha na si miaka 30.

"Mheshimiwa Hakimu, kwa mujibu wa kifungu hiki mfungwa aliyopo mbele ya mahakama yako tukufu anastahili kutumikia kifungo cha maisha gerezani na sio miaka 30," alisema.

Hakimu Singano alisema anakubaliana na hoja ya Mwanasheria wa Serikali na kumwongezea adhabu ya kifungo cha maisha gerezani badala ya miaka 30 aliyopewa na Mahakama ya Wilaya ya Nachingwea.

Awali, ilidaiwa kuwa Januari 10, 2023, Wilaya ya Nachingwea na Mkoa wa Lindi, alimwingilia kinyume na maumbile kijana huyo na kumsababishia maumivu makali sehemu ya siri.


**IN THE DISTRICT COURT OF LONGIDO AT LONGIDO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 25612 OF 2023**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE PATRICIA MICHAEL KIMOLO**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY SUZAN FLUGENS EMMANUEL**

**GENERAL CITATION**
**(Made Under Rule 75 of the probate Rules)**

All persons claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above – named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 22nd day of DECEMBER, 2023.
No will of the said deceased is deposed is deposited at the court.
DATED at LONGIDO this 15th day of DECEMBER, 2023.

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT - LONGIDO



**KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI**

**TANZANIA ENVIROMENT ACTION**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye usajili namba MC 264 BBY.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Polisi Taarifa:
**KIL/MOS/RB/387953/2022**



**MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA FINANCIAL SERVICES LTD, DENNESTO COMPANY LIMITED** tunautangazia umma kuwa tutauza kwa mnada wa hadhara Mali ya mdaiwa Sugu kama ilivyotangazwa gazetini

| Mdhamini /Mdaiwa | Dalali | Aina ya Mali /Mahali | Tarehe mnada |
|---|---|---|---|
| Vicent Ringson Mberesero | DENNESTO COMPANY LIMITED | Mitsubishi Canter T.682 DUC, Makumbusho Yard- Dar | 02 Jan 2024 |

Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi.

Gharama za kukagua na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga: -**
**DENNESTO- 058896226/070769777826**

# Vyakula vya stendi, barabarani vyaweka hatarini afya ya walaji

## -Madaktari bingwa, wanasheria watoa angalizo

**Na Mary Mosha,** MOSHI



Baadhi ya wafanyabiashara wakiuza vyakula na bidhaa zingine katika Stendi Kuu ya Mabasi Moshi wiki iliyopita kwa utaratibu unaolalamikiwa kukinzana na sheria na kanuni za usalama wa afya. **PICHA: MARY MOSHA**

SEHEMU ya kwanza ya ripoti hii jana, iliangazia ukiukwaji wa Sheria ya Afya ya Jamii ya Mwaka 2009 unaoshuhudiwa katika Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro; vyakula kuandaliwa katika mazingira hatarishi kiafya kisha kuuzwa kwa abiria wanaofika katika Stendi Kuu ya Mabasi Moshi na vichochoro vyake.

Katika toleo la pili la ripoti hii leo, wakazi wa Moshi wanasimulia kinachowasibu wanaokula vyakula hivyo huku wataalamu wa afya wakifafanua kitabibu athari zake kiafya. Sasa endelea...

Emmanuel Samson ni wakala wa mabasi katika Stendi ya Mabasi Moshi, analalamika kuwapo vyakula na vinywaji vingi visivyo na viwango katika eneo lake hilo la kazi.

Anadai vyakula na vinywaji hivyo ni vichafu na vimekuwa vinasababisha madhara kwa wananchi, lakini anainyooshea kidole serikali kwa kujikita katika ujenzi wa stendi za mabasi kila mkoa pasi na kudhibiti uuzwaji holela wa vyakula na vinywaji.

"Kuanzia mwaka jana (2022) tumezika watu wanane ambao walikula vyakula visivyo na ubora na wengine kunywa hizi pombe za kupima kwenye vikopo vidogo. Unaweza kusema siku zao zilikuwa zimefika, lakini mazingira pia yanachangia.

"Katika eneo la uchochoro wa Mawenzi, jirani kabisa na stendi hii, yupo mama ntilie mmoja mwaka 2020 alisababisha kifo kwa watoto wake wawili na mmoja wa jirani yake.

"Alirejea nyumbani akiwa na chakula kutoka kijiweni. Kilikuwa kidogo, akaamua kuwapitia watoto, yeye hakula, kiligeuka sumu (food poison), wale watoto walipoteza maisha.

"Licha ya tukio hilo, hakuna ofisa afya aliyefika hapa stendi kuu kutafuta utatuzi wa changamoto hii ya vyakula visivyo na ubora. Badala yake wamejikita katika kuchukua ushuru wa usafi katika maduka na kutoa vibali vya biashara," analalama.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani Hospitali ya Rufani ya Kanda KCMC, Elichilia Shao, anaanza kwa kutoa hadhari kwamba chakula kinachotengenezwa katika mazingira hatarishi, kinatengeneza sumu.

Katika hilo, Dk. Shao, anatoa fasili ya sumu kwamba ni kitu chochote kinachoingia mwilini na kusababisha mwili kushindwa kufanya kazi na kuleta madhara kwenye kinga ya mwili, kuharibu mmeng'enyo wa chakula na damu.

Takwimu za afya kutoka Kanzidata ya Mkoa wa Kilimanjaro zinaonesha kuwa hospitali mkoa huo kwa mwaka 2020, zilipokea wagonjwa 1,571 wa matukio ya sumu.

Kati yao, Manispaa ya Moshi wagonjwa 355, Wilaya ya Moshi 319, Siha 151, Hai 290, Rombo 195, Same 139 na Mwanga 122.

Kwa mwaka 2021, waliripotiwa wagonjwa 1,468. Kati yao, Manispaa ya Moshi 304, Wilaya ya Moshi 322, Siha 192, Hai 204, Rombo 202, Same 130 na Mwanga 114.

Mwaka uliofuata (2022), kanzidata hiyo inaonesha wagonjwa walioripotiwa ni Manispaa ya Moshi 298, Wilaya ya Moshi 443, Siha 367, Hai 238, Rombo 198, Same 93 na Mwanga 109.

Kwa mwaka huu, hadi kufikia Oktoba 2023, wagonjwa walioripotiwa ni Manispaa ya Moshi 435, Wilaya ya Moshi 271, Siha 314, Hai 138, Rombo 202, Same 106 na Mwanga 109.

Dk. Shao anasema sumu inapoingia mwilini huanza kuharibu kinywa, mfumo wa chakula, upumuaji kisha utengenezaji wa mkojo na damu, hali inayopelekea mtu kukosa chembechembe nyekundu za damu, chembe sahani na kinga ya mwili.

Anasema sumu pia inaweza kusababisha mtu kuvuja damu sehemu mbalimbali au damu kushindwa kuganda.

Dk. Shao anataja baadhi ya sumu ni pamoja na zinazotumika kuhifadhi mazao. Mtu akizinywa zinakatisha uhai.

Bingwa huyo anasema kuna sumu zinazotokana na kula chakula kilichochacha au kilichoandaliwa kwenye mazingira duni.

"Sumu zinapatikana katika njia nyingi zikiwamo vyakula vilivyokaa muda mrefu, hivyo kuharibiwa na vimelea, inaweza kuwa sumu kuvu inayopatikana kwenye nafaka, hasa mahindi na unga kama haukuhifadhiwa vizuri.

"Sumu nyingine ni ile inayotumika kwenye mimea kwa ajili ya kuua vijidudu, hii ikiingia kwenye chakula au maji lazima anayekula atapata madhara.

"Kama chakula kimepikwa na hakikuhifadhiwa vizuri kwenye hali ya baridi inayokubalika ili vimelea visizaliane au kutopashwa vizuri kabla ya kuliwa, kinaweza kumsababishia mtu madhara kama kutapika, kuharisha damu na hata kupoteza maisha asipopata matibabu kwa wakati," anaonya.

Dk. Shao anasema walaji wa vyakula vya aina hiyo wako hatarini kukumbwa na maradhi ya homa, mwili kutetemeka, maumivu ya kichwa, kutoka jasho kupita kiasi, kupata ganzi na kutembelewa na vitu wasivyoviona kwenye ngozi.

Pia anasema ulaji wa vyakula vya aina hiyo husababisha kupata kiu kali, wengine kupata udhaifu wa mwili na kizunguzungu.

Bingwa huyo wa KCMC anafafanua kuwa katika mfumo wa fahamu, mtu anaweza kupata shida ya kuona, kuwa zezeta, kupata ganzi kwenye miguu, matatizo ya moyo na misuli kushindwa kufanya kazi, kunakopelekea kulala chini mpaka atakapopata matibabu stahiki.

Dk. Shao anarejea taarifa za Shirika la Afya Duniani (WHO); zaidi ya watu milioni 600 duniani wanapata magonjwa yanayosababishwa na sumu/vimelea kila mwaka.

"Kwa Tanzania kuna utafiti ulifanyika Dodoma juu ya sumu kuvu kwenye mahindi, unga na ugali. Katika nyumba walizotembelea, walikuta zaidi ya asilimia 70 unga ulikuwa na sumu kuvu na asilimia 29 kwenye ugali, ilikuwa juu ya kiwango ambacho mwili una uwezo wa kuhimili," alisema.

Bingwa huyo anatoa angalizo kuwa ikiwa vyakula havitaandaliwa katika mazingira mazuri, safi na salama, ni rahisi kuchafuliwa na dawa au kugeuka sumu vinapotumiwa na hivyo kuleta madhara mengi kuanzia kupoteza fahamu, kutokuona, kuharisha na kutapika.

"Zipo sumu zinazosababisha ini na figo kushindwa kufanya kazi, hasa zile mtu anazotumia katika kujitoa uhai. Hawa kwa asilimia 90 hawaponi.

"Kwa sasa kutokana na mtindo wa maisha msongamano wa watu, madhara ya sumu yanazidi kuwa tatizo kubwa hasa kwa kuhifadhi chakula eneo lisilo salama au kuandaa chakula kwenye mazingira duni," anasema.

Nini kifanyike? Dk. Shao anasema ipo haja kutoa elimu kwa waandaaji wa chakula hasa mama lishe na baba lishe, wauzaji na watumiaji wenyewe ili kufahamu madhara yatokanayo na vyakula hivyo.

"Ni muhimu elimu hii itolewe ili kuongeza umakini na usafi, hivyo kupunguza vyakula vinavyotengeneza au kuwa na sumu inayodhuru mwilini," anashauri.

Ni hoja inayoungwa mkono na Mtafiti wa Mazingira ambaye ni Mhadhiri wa Mazingira katika Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, Dk. Mwema Mwema, ambaye pia ananyoosha kidole kwa wauzaji karanga wanaozifunga katika mifuko ya plastiki, wanasababisha sumu kuvu.

"Hawa wauzaji hufunga karanga zao katika vifungashio vya plastiki, hutembea navyo siku nzima, zinapopigwa na jua husasabisha unyevu ambao unaweza kupelekea sumu kuvu kwa karanga na hata korosho ambazo nazo zinauzwa kwa utaratibu huu," anaonya.

Dk. Mwema anaungana na mtangulizi wake Dk. Shao kuitaka jamii kubadili mfumo ya ulaji na namna ya kufungusha vyakula ili kupunguza madhara ya kiafya kwa watumiaji.

Mtaalamu wa Tiba Asilia, Lucia Moleli, anasema kinachoshuhudia katika stendi hiyo na maeneo jirani, ni matokeo ya mamlaka kutofanya ukaguzi wa mara kwa mara.

"Tunajua hawa wataalamu wa TBS (Shirika la Viwango Tanzania) hawawezi kufanya kazi hii wenyewe, wapo na mabwana afya na bibi afya katika kila kata na halmashauri. Hawaoni hali hii kweli?" anahoji.

Katika hilo, Ofisa Afya Mkoa wa Kilimanjaro, Happynus Kilula anatoa mrejesho kwamba ukaguzi unafanyika mara moja kila baada ya miezi mitatu na yapo mazingira ya kutoa onyo na kufungia wanaokaidi na hata kuwafikisha mahakamani wanaokiuka sheria.

"Kama kosa lililofanyika haliathiri afya ya watumiaji chakula hicho, tunatoa ilani ya kufungiwa na kupewa kibali cha kufanya marekebisho.

"Ikiwa chakula kinahatarisha afya ya jamii tunamchukulia hatua kwa kushirikiana na vyombo vingine likiwapo Jeshi la Polisi na mahakama," anasema Pilula.

Mratibu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) Ofisi ya Kanda ya Kaskazini, jijini Arusha, Wakili Hamis Mayombo anasema kufanya biashara ya chakula pasi na kufuata sheria na taratibu zinazoongoza biashara hiyo, ni kosa kisheria. Wanaokiuka sheria, washtakiwa kulingana na kosa lao.

"Ikiwa amesababisha mauaji kwa mujibu wa kosa hilo, na kama ni vinginevyo, basi atashtakiwa. Kwa vyovyote vile bado jambo hili si haki na ni onevu kwa watu wanaouziwa vyakula vyenye shida kiafya.

"Kuna haja ya serikali iangalie namna bora ya kusaidia jambo hilo hasa ikizingatiwa Sheria ya Afya ya Jamii ya Mwaka 2009 inaelekeza hatua za kuchukuliwa," Wakili Mayombo anashauri.

# Hoja wakulima alizeti yasikika serikalini

**Na Elisante John,** SINGIDA

SERIKALI imekubali ombi la muda mrefu la wakulima mkoani Singida kuhusu kupatiwa aina mpya ya mbegu ya alizeti (haysan) kwa bei ya ruzuku.

Mbegu hiyo ni yenye uwezo zaidi wa kuongeza uzalishaji shambani, ikitajwa kutoa mafuta ya kutosha baada ya alizeti kuchakatwa kiwandani.

Akizungumza na watendaji wa kata, vijiji na maofisa ugani wilayani Mkalama mwishoni mwa wiki waliokutana kwa ajili ya kuweka mikakati ya msimu mpya wa kilimo 2023/2024, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alisema ombi hilo limekubaliwa kwa manufaa ya taifa.

Alisema aina hiyo mpya ya mbegu itauzwa kwa bei ya ruzuku, lakini mkulima atalazimika kulipa fedha taslimu, ili kuepusha usumbufu kama ulivyotokea msimu uliopita. Baadhi ya wakulima waligoma kulipa mkopo, wakidai walipata hasara kwenye mavuno.

"Nendeni mkaitishe mikutano ya hadhara na waelezeni wakulima, serikali imekubali ombi lao la kupatiwa mbegu ya haysan na itaanza kusambazwa ndani ya wiki mbili kuanzia sasa, na itauzwa kwa bei ya ruzuku, lakini hii ni kwa fedha taslimu," alisema Serukamba.

Kwa mujibu wa Serukamba, Mkoa wa Singida ni tegemeo la mafuta ya kula nchini kupitia zao la alizeti, kutokana na takwimu kuonesha msimu uliopita 2022/23, Singida ilichangia asilimia 50 ya alizeti yote iliyozalishwa nchini.

Mkuu wa Mkoa alisema mbegu aina ya haysan ni suluhisho la mkulima nchini, baada ya kupaza sauti kiasi cha kutosha juu ya ubora hafifu wa mbegu aina ya awali (aliitaja kwa jina), ikiwa na mavuno haba, pia mafuta kidogo baada ya kuchakatwa kiwandani.

Katika hatua nyingine, Serukamba amewataka watendaji na wataalamu wa ugani kusimamia na kutoa elimu ya kutosha kwa wakulima kuhusu mbinu, kanuni na taratibu bora za kilimo, ili uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara uongezeke kwa lengo la kuwakwamua kiuchumi.

Kikao hicho kilikuwa mahususi kwa wataalamu wa ugani na watendaji wa kata na vijiji, pamoja na mambo mengine, kuandaa mikakati ya pamoja ili kuboresha kilimo, ikiwamo kuongeza eneo la uzalishaji mazao ya chakula na biashara mkoani Singida.

Kupitia makubaliano yao, waliazimia eneo la kilimo msimu huu wa 2023/24 katika wilaya hiyo, liongezwe ekari 9,940 zaidi, ili kuongeza mazao mbalimbali, yakiwamo ya chakula na biashara.

Katika msimu wa kilimo 2022/23, Wilaya ya Mkalama ililima eneo lenye ukubwa wa ekari 354,230.

Katibu Tawala Msaidizi Uchumi na Uzalishaji Mkoa wa Singida, Stanslaus Choaji, aliwataka washiriki wakasimamie vyema kilimo bora, sambamba na kuwasimamia wakulima waliopatiwa mbegu ya alizeti msimu uliopita, warejeshe madeni yao.

Choaji alisema kuwa dawa ya deni ni kulipa, kuacha kulipa ni kosa kisheria, hivyo wote waliokopeshwa mbegu ya ruzuku msimu uliopita, wanapaswa kulipa badala ya kugoma, ili serikali iendelee kuwapatia mbegu bora na mbolea kuongeza uzalishaji.

"Kimsingi, ni majukumu yetu hapa sote kwenda kufanikisha suala hili. Kwa hiyo, tunaipongeza serikali na ninaamini kutokana na kikao hiki, sasa tunakwenda kusimamia zoezi hili, ili wakulima waweze kunyanyuka kiuchumi," alisema Choaji.

Baadhi ya wananchi wa halmashauri za Singida na Mkalama walipongeza juhudi za serikali na kufafanua kuwa wanaamini wataanza kunufaika na kilimo cha alizeti kwa kuzalisha mafuta mengi zaidi.

Mmoja wa wakulima hao kutoka kijijini Ngimu, Ramadhan Ng'imba, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Uwajibikaji na Ufuatiliaji (SAM), Kata ya Ngimu, aliishukuru serikali kwa kufanikisha mpango huo, lakini akaomba iwasamehe deni la ruzuku la mwaka jana kutokana na mbegu waliyopanda kutokuwa na mavuno ya kutosha.




Waziri wa Maji, Jumaa Aweso (kushoto), akimsikiliza Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Kiula Kingu, akielezea mradi wa kusambaza majisafi kwa wananchi wa Mkoa wa Pwani na Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Kibaha. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Aweso aagiza kutumika mita malipo kabla ya kutumia maji

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, ameitaka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kwenda na kasi ya mabadiliko ya teknolojia kwa kuanza kutumia mita za malipo ya kabla ya matumizi ya maji.

Aliagiza hayo mwishoni mwa wiki wakati wa hafla ya kutia saini makubaliano ya utekelezaji miradi ya maji kati ya DAWASA na Kampuni ya Shanxi, wilayani Kibaha, mkoani Pwani.

Kukamilika kwa miradi hiyo ya maji yenye thamani ya Sh. bilioni 48 kunatarajiwa kuimarisha uchumi wa viwanda mkoani Pwani kutokana na uhakika wa upatikanaji majisafi kwenye maeneo ya viwanda.

Waziri Aweso alisema mita za kulipa kabla ya matumizi zitasaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa malalamiko ya wananchi kuhusu bili za maji na wengine kudai kupewa bili kubwa kuliko matumizi yao.

Alisema wataalamu wa Wizara ya Maji wanapaswa kuweka mikakati ya kuhakikisha wanaondokana na utaratibu wa sasa wa kulipa bili baada ya matumizi ya maji.

"Huu ni wakati sahihi kwa DAWASA na mamlaka zingine kuanza kutumia teknolojia hii ya mita za kulipa kabla kwa sababu zitasaidia kuleta mageuzi nchini kwenye utoaji huduma ya maji kwa wananchi," alisema Aweso. Aliitaka DAWASA kuhakikisha inasimamia kwa karibu miradi hiyo ya maji ya Pangani, Kimbiji mpaka Chuo cha Uhasibu na Kwala kwa ufanisi ili iwe na tija kwa wananchi na kukuza uchumi wa viwanda kwa Mkoa wa Kibaha.

Aweso alisema miradi hiyo ni tegemeo kubwa kwa wakazi wote pamoja na kukuza maendeleo ya Mkoa wa Pwani na maeneo ya Dar es Salaam, hivyo mkandarasi anatakiwa asimamiwe kwa karibu ili tija ya miradi ionekane kwa wananchi.

Waziri Aweso alieleza kuwa miradi hiyo ikikamilika, kusiwe na usumbufu katika kuunganisha wananchi kwenye huduma kwa kuwa ni haki ya kila mmoja kupata huduma ya majisafi kwa wakati, akiwataka wananchi nao watimize wajibu wao kwa kulipa bili kwa wakati.

"Mwananchi anapaswa kushirikishwa kwa ukaribu kujua kiwango cha maji alichokitumia ili ajue bili anayopaswa kulipa, wasomamita washirikishe wananchi wakati wa usomaji mita," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Aboubakar Kunenge, alisema kupitia utekelezaji miradi mbalimbali ya majisafi Mkoa wa Pwani, upatikanaji maji mkoani mwake umefikia wastani wa asilimia 86 na juhudi zinaendelea za kuboresha huduma.

"Tunaridhishwa na jitihada za DAWASA katika uboreshaji huduma na tuna imani kwa kasi hii tutaweza kufikia asilimia 95 ya upatikanaji huduma kufikia mwaka 2025," alisema Kunenge.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Kiula Kingu, alisema kwa ujumla ya miradi mitatu ikiwamo miradi ya Kwala, Pangani na Kimbiji mpaka Chuo cha Uhasibu, imetiwa saini kwa lengo la kuboresha huduma kwa Mkoa wa Pwani na Dar es Salaam. Alisema miradi hiyo inatekelezwa kwa fedha za Serikali Kuu na DAWASA Sh. bilioni 48. Mradi wa maji Pangani utanufaisha wananchi 14,868 wa maeneo ya Kibaha - Msufini, Lulanzi, Tamco na Pangani.

Mradi wa maji Kimbiji mpaka Chuo cha Uhasibu unalenga kunufaisha wakazi wa Tazara, Ukonga mpaka Gongo la Mboto wakati mradi wa Kwala utanufaisha wananchi 7,901 wa Bandari Kavu pamoja na vitongoji vya Kwala.

## Benki ya Stanbic yatoa msaada wa mil. 10/- waathirika Katesh

**Na Jenifer Gilla**

BENKI ya Stanbic imetoa msaada wa vyakula vyenye thamani ya Sh. milioni 10 kuwasaidia waathirika wa maporomoko ya tope, mawe na magogo katika mji wa Katesh, wilayani Hanang, mkoani Manyara.

Msaada huo unatolewa ikiwa wiki moja tangu Rais Samia Suluhu Hassan kutoa wito kwa taasisi binafsi, mashirika na Watanzania kwa ujumla kuendelea kutoa michango kwa namna watakavyoguswa ili kuwasaidia waathirika hao warudi katika maisha yao ya awali kwa kuwa mahitaji bado ni mengi.

Jumla ya kaya 107 zilizokuwa na wakazi 322 zimepoteza makazi na mali zao katika maeneo ya Katesh na Gendabi kutokana na maporomoko ya matope yaliyosababishwa na mvua iliyonyesha usiku wa kuamkia Desemba 3, mwaka huu.

Mkurugenzi wa Kitengo cha Wateja Binafsi wa Benki ya Stanbic Tanzania, Omari Mtiga, alisema jana kuwa wametoa msaada huo kumuunga mkono Rais Samia aliyechukua hatua za haraka kuwasaidia wananchi waliokumbwa na maafa hayo yaliyosababisha vifo vya watu 89 na wengine wengi kujeruhiwa.

Aliitaja misaada waliyoitoa ni mchele, unga, maharage na mafuta, vyote thamani yake ni shilingi milioni 10.

Alisema mbali na kutoa msaada huo, viongozi wa benki hiyo pia walitembelea maeneo yaliyoathiriwa zaidi na maporomoko hayo katika mji wa Katesh kushuhudia hali ilivyokuwa na kuzungumza na waathirika wa mafuriko hayo wakiwamo wafanyabiashara.

"Hii ni moja ya shughuli za kijamii zinazopewa kipaumbele na taasisi hii inayoamini kuwa na mchango mkubwa katika jamii ili kuleta maendeleo ya nchi," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang', Francis Namaumbo, aliishukuru benki hiyo kwa kutoa msaada huo na kusema serikali itasimamia kikamilifu ili misaada hiyo iwafikie walengwa.

Desemba 10, mwaka huu, wakati akipokea msaada wa fedha kutoka kwa mashirika ya umma, Rais Samia alisema misaada inayoendelea kutolewa ikiwamo vifaa vya ndani, vyakula na huduma za afya ni faraja kubwa kwa wananchi hao wanaopitia kipindi kigumu cha kupoteza ndugu na mali zao.

Alisema fedha zinazokusanywa, zitatumika kujenga nyumba ili kuwarudishia wananchi hao faraja kwa kile walichopoteza na waendelee na maisha yao kama kawaida.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga mechi Wydad, Medeama ziwe fainali kwenu

**MIAMBA** ya Tanzania, Simba na Yanga, ambao ni wawakilishi pekee wa nchi kwenye michuano ya kimataifa kwa ngazi ya klabu Afrika, kesho na keshokutwa, Jumatano zitashuka Uwanja wa Benjamin Mkapa, kuzikaribisha Wydad Casablanca ya Morocco na Medeama ya Ghana.

Katika mechi hizo za raundi ya nne ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kesho Simba itakuwa mwenyeji wa Wydad, wakati keshokutwa, Jumatano Yanga ikiikaribisha Medeama, mechi zote zikipigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Wawakilishi hao wa Tanzania, Simba na Yanga wote wanaburuza mkia kwenye makundi yao, kila moja ikiwa na pointi mbili mkiani mwa Kundi B na D, hivyo ushindi pekee katika michezo yao kesho na keshokutwa ndio utakaozirejeshea matumaini ya kufuzu robo fainali.

Lakini pia zikipoteza, safari yao ya kurejea kujiandaa tena kwa michuano hiyo msimu ujao, itakuwa imeanzia hapo, hivyo hizo ni mechi muhimu kwao kucheza kama fainali ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele, kitu ambacho ndio matarajio makubwa kwa Watanzania wote kuona kikitokea.

Kama zitapata ushindi ina maana kwa Simba itafikisha pointi tano na kupanda hadi nafasi ya pili kwenye Kundi B, lakini ikitegemeana na matokeo kati ya Asec Mimosas itakayokuwa nyumbani Ivory Coast kuikaribisha Jwaneng Galaxy ya Botswana.

Asec inaongoza Kundi B ikiwa na alama saba ikifuatiwa na Jwaneng Galaxy yenye pointi nne huku Wydad ikiwa na pointi tatu na Simba mbili. Kwa mantiki hiyo kinachotakiwa ni Simba kushinda wakati huohuo Asec nayo ishinde.

Kwa upande wa Yanga nayo keshokutwa kama itapata ushindi itafikisha pointi tano, lakini kupanda kwao nafasi ya pili kutategemea pia na matokeo kati ya Al Ahly ya Misri ambayo itakuwa ugenini nchini Algeria dhidi ya Belouizdad.

Ikumbukwe Al Ahly inaongoza msimamo wa Kundi D ikiwa na pointi tano ikifuatiwa na Belouizdad yenye alama nne sawa na Medeama, hivyo nalo ni kundi gumu, ila kwa Yanga kinachotakiwa ni kushinda tu mechi zake bila kutazama matokeo ya mwingine.


Kimahesabu Simba na Yanga zote zina nafasi sawa ya kutinga robo fainali kama zitaweza kuutumia vema uwanja wa nyumbani katika michezo yao miwili zilizobakiza kila moja huku mechi moja ya ugenini zikijitahidi angalau kwenda kulazimisha sare.

Kinachotakiwa kwa wawakilishi hao wa nchi ni kucheza mechi zao za nyumbani kama fainali kwa kila mchezaji kujitoa kwa kuhakikisha wanavuja jasho haswa mwanzo mwisho wa mchezo, pia bila kuwakosea heshima wapinzani wao.

Lakini kwa mashabiki wa soka na Watanzania kwa ujumla wanapaswa kuwq mstari wa mbele katika kwenda uwanjani kuzisapoti timu zao mwanzo mwisho wa mchezo ili kuwaongezea ari ya ushindi wachezaji wanapopambana dimbani.

Tunaamini Simba, Yanga zina wachezaji wa daraja la juu kabisa ambao wanaweza kubadili matokeo muda wowote na kuzisaidia timu zao kupata alama tatu katika mechi hizo, hivyo ni wakati sasa kila mmoja kuwajibika ipasavyo katika nafasi yake kuanzia nje hadi ndani ya uwanja ili kupata ushindi kwenye michezo hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Simba itumie hali ya hewa, Yanga mashabiki kushinda mechi zao CAF

Na Adam Fungamwango

**KUNA** faida ambayo haionekani sana kwenye macho ya kawaida kwa Simba na Yanga ambazo kesho na Jumatano zitacheza mechi zao za Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi dhidi ya Wydad Casablanca ya Morocco na Medeama ya Ghana.

Simba itacheza mechi yake ya raundi ya nne kesho dhidi ya Wydad Casablanca kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, saa 10:00 jioni. Ni muda ambao kwa hapa Tanzania kunakuwa na joto ambalo huzisumbua sana timu za Afrika Kaskazini.

Kwa uchunguzi wangu mdogo ni kwamba timu za ukanda huo maarufu kama za Waarabu zinaathirika sana zinapocheza mechi zake hapa nchini muda wa saa 10:00 jioni na imekuwa mara chache sana kupata ushindi.

Katika mechi zake zote mbili Simba iliposhinda bao 1-0 dhidi ya Al Ahly mechi za makundi Ligi ya Mabingwa 2019 kwa bao la Meddie Kagera na 2021 kwa bao la Luis Miquissone, mechi zote hizo zilicheza saa 10:00 jioni.

Biashara United iliifunga Al Ahli Tripoli ya Libya mabao 2-0 kwenye Kombe la Shirikisho, Oktoba 15, Uwanja wa Benjamin Mkapa, mechi hiyo ilichezwa saa 10:00 jioni.

Septemba 17, mwaka huu, Singida Fountaine Gate, ikicheza Kombe la Shirikisho, iliifunga Future ya Misri bao 1-0, katika mechi ambayo kama ingetulia, basi Singida ingeweza kupata mabao mengi sana.

Ukiangalia kwa makini ni kwamba wachezaji wa timu pinzani wanakuwa wamechoka kutokana na joto kwa sababu wao hawajazoea hivyo, mara nyingi mechi zao huchezwa usiku, saa 1:00 au 4:00 kwa saa za Afrika Mashariki.

Februari 18, mwaka huu, Simba ilishindwa kuifunga Raja Casablanca, badala yake ikabugizwa mabao 3-0, moja ya sababu nyingine ni kwamba mechi ilichezwa usiku, sina shaka ingekuwa saa 10:00, jamaa wangeonja pumzi ya moto.

Kwa maana hiyo, mechi ya kesho kuchezwa saa 10:00 jioni ni faida kubwa kwa Simba kama makocha na wachezaji watakuwa na mipango mikakati kwa ajili hiyo. Hata kama kutakuwa na mawingu au mvua ikanyesha kidogo, lakini haiondoi kuwapo kwa hali ya joto la Dar es Salaam ambalo linawasumbua mpaka wakazi wenyewe.

Wachezaji wa Simba kama wamefanyia kazi hali hiyo ya hewa na kuamua kuwapeleka mputa mputa wapinzani wao, nina uhakika kila dakika zinavyozidi kwenda mbele ndiyo watakavyokuwa na uwezekano wa kupata mabao.

Kwenye joto wachezaji wa Afrika Kaskazini wanachoka sana. Kwanza huwa hawachezi kwa kasi kama ilivyo kawaida yao, na ukiwapiga presha ya nguvu wanachanganyikiwa na wanazidi kutepeta. Kifupi tu, wachezaji wa Simba katika mechi hiyo muhimu wasifuatishe mpira wa Wydad Casablanca ambao watataka kuupoozesha.

Kinachotakiwa ni kuwachezesha kwa kasi mwanzo hadi mwisho na nina uhakika wakifanya hivyo, ushindi utapatikana.

Kwa upande wa Yanga, wao wamekuja na mbinu ya kununua tiketi zote eneo la mzunguko. Kinachotakiwa ni mashabiki kwenda uwanjani kwa wingi na kushangilia mwanzo hadi mwisho katika mechi ya Jumatano dhidi ya Medeama.

Duniani kote inaeleweka kuwa mashabiki ni mchezaji wa 12, ambao wana nafasi yao kwenye soka. Pamoja na kwamba mashabiki hawaleti ushindi moja kwa moja kwani timu zimekuwa zikifungwa na mashabiki wao uwanjani, lakini mara nyingi wingi na ushangiliaji umekuwa ukiwapa wapinzani wakati mgumu.

Kumbuka kipindi ambacho Simba inajaza Uwanja wa Banjamin Mkapa katika mechi zake za kimataifa, wapinzani walikuwa wakiogopa kucheza uwanja huo ulioonekana kama 'machinjio' kwao.

Hata timu kubwa zenye mashabiki wengi kama Al Ahly, Zamalek, Orlando Pirates, Kaizer Chiefs na nyingine nyingi zinaugwaya uwanja huo kutokana na kufurika mashabiki na ushangiliaji wao. Mashabiki wa Yanga kama wataujaza na kuishangilia timu yao kwa nguvu, wanaweza kuisaidia kwa kiasi kikubwa kuibuka na ushindi.

Kumbuka kuwa mechi hizo ndizo zitakazoamua mustakabali wa timu za Tanzania kwenye michuano hiyo msimu huu.

## HABARI KITAIFA

# Serikali yajivunia huduma kwa waathirika maporomoko Hanang'

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imesema inajivunia kutekeleza wajibu wake katika kukabiliana na maafa yaliyotokana na maporomoko ya tope, magogo na mawe yaliyotokea katika mji wa Katesh, wilayani Hanang, mkoani Manyara mwanzoni mwa mwezi huu.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, alisema mwishoni mwa wiki kuwa tayari serikali imeanza kurejesha hali nzuri kwa wananchi wa maeneo hayo kwa kuwapatia misaada ya vyakula na huduma nyingine za kijamii.

Alitoa kauli hiyo mjini Morogoro alipofungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu kilicholenga kujadili taarifa ya Bajeti ya 2023/24 ya ofisi hiyo.

Alisema serikali chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imefanya kazi kubwa ya kukabili maafa hayo kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu.

Waziri huyo alisema Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) inaendelea kushughulikia maafa yaliyotokea wilayani Hangang, akisisitiza kuwa imejipanga na ina uwezo wa kujiratibu yenyewe na kufanya uratibu wa mambo mengine ya kitaifa. Sasa inaendelea kushughulikia maafa ya Hanang kwa nguvu kubwa.

Alisema Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na timu mbalimbali, imefanikiwa katika kushughulikia maafa hayo na Rais ameridhishwa na hatua zilizochukuliwa.

Akizungumzia umuhimu wa baraza hilo, waziri huyo aliwataka wajumbe wake na watumishi kufanya kazi kwa kutegemeana na kushirikiana bila kutengeneza makundi.

Waziri Jenista alisema kuna kila sababu kufanya uamuzi wa pamoja wa ushirikishwaji ili kupata mafanikio kwenye idara na vitengo kama viongozi wa juu wanavyofanya kazi vizuri kwa kushirikiana.

Alisema kuwa hata kama inafikia wakati mtendaji hayupo kwenye Idara au kitengo, kuwe na mtu anayeweza kufanya kazi kwa viwango na uwezo huohuo ili mambo yaweze kwenda vizuri.

Alisema anafarijika na utendaji wa kitaasisi na kuwaomba watumishi kuendelea kuimarisha utendaji wa kitaasisi ambao unatoa fursa kwa kila mtu kuwa sehemu ya mafanikio na ufanisi wa taasisi.

"Viongozi wenzangu wenye madaraka kwenye idara, vitengo au taasisi zetu, mhakikishe mnajenga moyo wa kukuza watumishi walio chini yenu, kwa kuwapa fursa ya kukua kielimu ndani ya ofisi, kukua kiujuzi na kukua kiubobezi," aliagiza.

Waziri Jenista alisema watumishi wa umma ni rasilimali muhimu ya kuendesha rasilimali nyingine na kusema kuwa ni lazima kuiratibu vizuri rasilimali hiyo na kuilinda kwa nguvu zote ili kupata mafanikio waliyokusudia.

Alitolea mfano Rais wa awamu ya tatu, Hayati Benjamin Mkapa aliwahi kusema, 'jambo muhimu kwa mfanyakazi si muda anaotumia kufanya kazi, bali kiasi cha kazi anachoweza kufanya katika muda aliopewa'.

Hivyo, Jenista alisema kuna kila sababu ya kuanza kujipima wenyewe kuanza mwakani, ili kujua kiasi cha kazi walizofanya na ufanisi wake kila siku wakati katika Ofisi ya Waziri Mkuu.

Katibu Mkuu katika ofisi hiyo, Dk. Jim Yonazi, alisema vikao vya wafanyakazi ni tamko la kisheria ambalo chimbuko lake ni Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, alilolitoa katika tamko Na. 1 la mwaka 1970 linalohimiza ushirikishwaji kupitia Baraza la Wafanyakazi.

Awali akitoa salamu, Katibu wa TUGHE wa Mkoa wa Dodoma, Samwel Nyungwa, aliipongeza Menejimenti ya Ofisi ya Maziri Mkuu kwa kutekeleza kikamilifu sera ya ushirikishwaji, akisisitiza "hakuna haki bila wajibu".

Alisema, "kama chama na sisi tunaangalia wafanyakazi wanavyopata haki na pia namna ambavyo wao wanatekeleza wajibu katika kuhakikisha mipango iliyopangwa inakamilika."



Uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke; Mstahiki Meya, Abdallah Mtinika (kulia), Mkuu wa Wilaya, Sixtus Mapunda na Mkurugenzi, Elihuruma Mabelya, wakiwa pamoja na wawakilishi kutoka taasisi za serikali zilizoshiriki kongamano la fursa za uwekezaji katika ukumbi wa DYCC Chang'ombe jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

HARUFU YA RUSHWA

# Mchengerwa atishia kusitisha vikao mabaraza ya madiwani

**Na Augusta Njoji,** GEITA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa ametishia kusimamisha vikao vya mabaraza ya madiwani iwapo watabainika kujihusisha na vitendo vya rushwa na kufanya uamuzi kinyume cha taratibu.

Mchengerwa akizungumza na watumishi wa halmashauri za Mkoa wa Geita katika ziara yake ya kukagua miradi ya maendeleo mwishoni mwa wiki, aliwataka madiwani kujiepusha na rushwa kwa kuwa inasababisha mambo mengine kuharibika kwenye halmashauri zao.

"Madiwani kuna uamuzi mnayafanya kinyume cha taratibu, acheni! Mmepitisha kwenye baraza mmeweka mwekezaji kwenye eneo ambalo ni la wazi.

"Niwaombe sana, fanyeni uamuzi kwa mujibu wa taratibu. Kule Bukoba niliwaambia jana wanachelewesha mipango ya miradi ya maendeleo kwa sababu za kisiasa. Nimewaambia kwa sababu mamlaka ninayo, nitasimamisha mabaraza ya madiwani ili maendeleo yanayopaswa kufanyika kwa wananchi yafanyike," alisema.

Alisema serikali inatoa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji miradi ambayo inahitaji usimamizi mzuri ili kuwa na tija kwa Watanzania.

"Niwaambie tu TAMISEMI inabeba zaidi ya asilimia 76 ya watumishi wote wa umma nchini na TAMISEMI inabeba asilimia 25 ya bajeti yote ya serikali. Inahitaji watumishi kufanya kazi kwa bidii kujitoa kwa ajili ya Watanzania," aliagiza.

Vilevile, waziri huyo alimwagiza Meneja wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) mkoani humo hakikisha anapitia maeneo yote na kupeleka mpango kazi ili TAMISEMI ione namna ya kupata fedha ili barabara zipitike vizuri.

"Mpango wetu wa serikali ifikapo mwaka 2025 tuwe tumetekeleza ilani ya CCM asilimia 85 ya uboreshaji barabara zetu za mijini na vijijini," alisema.

Waziri Mchengerwa pia alisema kuwa kutokana na kuwapo na matumizi ya ovyo ya fedha za miradi kunakosababisha miradi kutokamilika kwa wakati, TAMISEMI inakuja na utaratibu mpya wa kuzibana halmashauri kwa kuweka sharti la kutia saini fomu maalum inayolenga miradi kutekelezwa kwa wakati kwa fedha zilizotengwa.

"Tunakuja na mpango wa maboresho ambayo yanatoa sharti kwa mkurugenzi wa halmashauri, mhandisi na ofisa ununuzi kutia saini ili kujifunga kuwa watakamilisha mradi husika kwa wakati na kwa fedha walizotenga.

"Kumekuwa na utaratibu serikali inaleta fedha, mfano fedha za kujenga kituo cha afya Sh. milioni 500, baadaye tunaambiwa kuna uhitaji wa fedha za nyongeza Sh. milioni 200 kwa kuwa fedha haitoshi," alisema.

Waziri Mchengerwa pia alimwagiza Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martin Shigela, kuchunguza tuhuma zinazomkabili Ofisa Mifugo mkoani humo, anayedaiwa kukamata mifugo na kutoza faini bila kutoa risiti za serikali. "Ofisa huyu anakamata mifugo, anatoza fedha haziingii serikalini, hatoi risiti za serikali.

Hatuwezi kuruhusu mambo haya yaendelee. Rais Samia Suluhu Hassan amekataa dhuluma, hivyo tuwatendee haki Watanzania, wafugaji wana haki ya kuishi kama wengine," alionya.

Mbunge wa Geita, Joseph Musukuma, alimshukuru Rais Samia kutokana na serikali yake kupeleka fedha za miradi kwenye majimbo yote nchini.

Ni hatua ambayo ni matakwa ya kikatiba, hata hivyo. Ibara ya 8(1)(c) ya Katiba ya nchi inaitaka serikali kuwajibika kwa wananchi.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Mfanyabiashara kizimbani mashtaka uhujumu uchumi, hasara bil. 1/- TRA

**Na Grace Gurisha**

MKURUGENZI wa Kampuni ya Wintech (T) Ltd, Emmanuel Nkalang'ano (50), amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam, akikabiliwa na mashtaka manane likiwamo la kuisababishia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) hasara ya zaidi ya Sh. bilioni moja.

Mbali na Nkalang'ano ambaye ni mkazi wa Temeke, washtakiwa wengine ni Rugainunula Lwekamwa (53), mkazi wa Temeke na Mwita Nyakiha (55), mkazi wa Goba, wilayani Ubungo.

Walifikishwa mahakamani mwishoni mwa wiki mbele ya Hakimu Mkazi Joyce Mushi kujibu tuhuma zinazowakabili.

Washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka ya uhujumu uchumi ambayo ni kuongoza genge la uhalifu, kutoa risiti za uongo, kutumia kifaa cha kielektroniki kwa kupotosha mfumo, kuisababishia mamlaka husika hasara na utakatishaji fedha.

Wakili wa Serikali Mwandamizi Medalakini Emmanuel, akisaidiana na Jeniva Rugalama na Auni Chilamula, alidai kuwa katika shtaka la kwanza, tarehe tofauti kati ya Agosti 2022 na Agosti 2023, washtakiwa wakiwa eneo la Kariakoo, ndani ya Wilaya ya Ilala, mkoani Dar es Salaam, walipanga njama za uhalifu kwa kutoa risiti za uongo kwa nia ya kujipatia faida.

Alidai kuwa katika tarehe tofauti kati ya Agosti 2022 na Desemba 2022, washtakiwa wakiwa eneo la Kariakoo, Dar es Salaam, kwa pamoja walitoa risiti za uongo katika mashine ya vartual fiscal device iliyosajiliwa kwa jina la Rugainunula Lwekamwa kwa nia ya kumdanganya Kamishna Mkuu wa TRA kuwalipa walipakodi wengine Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) Sh. milioni 150. 9.

Ilidaiwa kuwa kati ya Januari 2023 na Agosti 2023, washtakiwa wakiwa eneo hilo hilo, walitoa risiti za uongo kutoka kwenye mashine hiyo iliyosajiliwa kwa jina la Rugainunula Lwekamwa kwa nia ya kumlaghai Kamishna Mkuu wa TRA ili kuwalipa walipakodi wengine VAT ya Sh. bilioni 1.1.

Alidai kuwa katika shtaka la kutumia vifaa vya kielektroniki kwa njia ya kupotosha mfumo, ilidaiwa washtakiwa wote kati ya Agosti 2022 na Desemba 2022, wakiwa eneo hilo, walitumia mashine ya vartual fiscal device iliyosajiiwa kwa jina la Rugainunula kutoa risiti za uongo za fedha zilizopakiwa katika mfumo wa TRA ili kuwaongezea walipakodi wengine kudai marejesho ya VAT ya Sh. milioni 150. 9.

Ilidaiwa kuwa kati ya Januari 2023 na Agosti 2023, washtakiwa, wakiwa katika eneo hilo, walitumia mashine hiyo iliyosajiliwa kwa jina la Rugainunula kutoa risiti za uongo zilizopakiwa katika mfumo wa TRA, hivyo kusababisha walipakodi wengine kudai marejesho ya VAT ya Sh. bilioni 1.16.

Katika mashtaka ya kuisababishia hasara mamlaka hiyo, washtakiwa wote wanadaiwa kwa tarehe tofauti kati ya Agosti 2022 na Desemba 2022, kwa makusudi waliisababishia TRA hasara ya Sh. 150,987,915.31. Kutokana na hali hiyo waliisababishia TRA hasara ya Sh. bilioni 1.16.

Wakili alidai kuwa katika tarehe hizo na eneo hilo, washtakiwa walifanya muamala wa fedha wa Sh. milioni 150. 9 huku wakijua kuwa fedha hizo ni zao la uhalifu, pia walijihusisha na muamala wa Sh. bilioni 1.16 huku wakijua kuwa fedha hizo ni zao la uhalifu.

Baada ya washtakiwa kusomewa mashtaka yao, Hakimu Mushi aliwataka kutojibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi na haina mamlaka ya kutoa dhamana kwa sababu mashtaka ya utakatishaji fedha hayana dhamana.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Desemba 28 mwaka huu itakapoitwa tena kwa ajili ya kutajwa.



Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Faustina Ndunguru (wa pili kulia), akitoa elimu ya usalama barabarani kwa watumiaji wa barabara na hasa wapanda pikipiki wakati wa kampeni ya Okoa Maisha iliyoandaliwa na Kampuni ya Bia Tanzania (TBL), Ubungo, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kulia ni ASP Mwashamba Onesmo aliyeshiriki utoaji elimu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Abiria waonywa ushabiki kwa madereva wazembe

**Na Said Hamdani,** LINDI

MWENYEKITI wa Usalama Barabarani (RSA) Kanda ya Kusini amewataka wananchi wa mikoa ya Lindi na Mtwara kuacha tabia kushabikia madereva wanaoendesha vyombo vya moto kwa mwendo kasi, badala yake watoe taarifa kwa vyombo vyenye mamlaka husika ili sheria ichukuwe mkondo wake.

Nassoro Mansour alitoa rai hiyo jana mjini hapa wakati wa utoaji elimu ya usalama barabarani kwa abiria wa mikoa hiyo.

Manzurui alisema kuwa hivi kuna tabia ya baadhi ya abiria kushabikia madereva wanaoendesha magari kwa mwendo kasi bila kufikiria athari zinazoweza kujitokeza mbele yao, ikiwa ni pamoja na vifo au kupata ulemavu wa kudumu.

Alisema kitendo cha kushabikia mwendo kasi ni kosa na hatari. Ni uvunjifu wa sheria za usalama barabarani kwa sabahu kinaweza kusababisha vifo na ulemavu.

Alisema wapo baadhi ya watu wamekuwa na kasumba kukataa magari yasiyokuwa yanakwenda mwendo kasi kwa madai ya kuchelewa kufika waendako bila kujali kwanza usalama wa maisha yao.

"Wapo baadhi ya abiria wamekuwa na kasumba, gari lisilokimbia kwa mwendo kasi hawapandi bila kuangalia athari zake zitakazotokea mbele yao," alisema.

Aliwataka abiria na wasio abiria kutoa taarifa kwa askari wa usalama barabarani pale wanapobaini uvunjifu wa wa usalama unaofanywa na madereva wasiofuata kanuni na sheria za kuendesha magari. Mwenyekiti huyo alisema ajali za barabarani kila mwaka zinachukuwa uhai wa watu wasiopungua milioni 1.35 na kuacha familia zikiwa na ukiwa.

"Leo hapa tulipo tunapoongea na ninyi hakuna mtu asiyepoteza ndugu yake kwa ajali za barabarani," alionya mwenyekiti huyo.

Alisisitiza wananchi wakiwamo abiria na wasio abiria kutokaa kimya pale wanapoona na kubaini uvunjifu wa sheria za usalama barabarani, badala yake watoe taarifa kwenye mamlaka husika.

Baadhi ya abiria walikuwa wanasafiri waliokuwa wanatoka na kuingia mikoa ya kusini; Lindi na Mtwara jana, wamewapongeza askari wa usalama barabarani kwa uangalifu wanaofanya licha ya kuwapo kasoro kadhaa.

# Manispaa ya Temeke yaanika fursa uwekezaji

**Na Joanita Joseph**

HALMASHAURI ya Manispaa ya Temeke kwa kushirikiana na wadau, imefanya kongamano la fursa za uwekezaji kwa lengo la kuwafahamisha wawekezaji, wafanyabiashara na wadau wa maendeleo kuwapo fursa mbalimbali za kiuwekezaji katika manispaa hiyo.

Vilevile, kongamano hilo lililofanyika mwishoni mwa wiki, lililenga kutoa elimu kuhusu uwekezaji na kujadili na kuweka maazimio kati ya wawekezaji na manispaa kuhusu uwekezaji.

Katika hotuba yake wakati wa kongamano hilo, Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Sixtus Mapunda ambaye alikuwa mgeni rasmi, alisema serikali inahitaji nguvu ya uwekezaji ili ikusanye mapato na kutoa huduma bora kwa wananchi.

"Serikali ili ifanye kazi vizuri, inahitaji ushiriki wa karibu sana wa sekta binafsi, ndio maana leo (Ijumaa) Manispaa ya Temeke imeona ni busara tukutane hapa tujadiliane changamoto zinazotukabili, tupeane fursa zilizoko na ninyi wawekezaji mtusaidie kutupa maneno ya busara na hekima namna bora ya kufanya mazuri zaidi," alisema.

Mapunda alitoa wito kwa wawekezaji kutumia fursa zilizoko Temeke za uwekezaji na kuwahakikishia ushirikiano pamoja na mazingira bora yanayofaa kwa uwekezaji.

"Ujio wa bandari mpya utabadilisha Jiji la Dar es Salaam. Kwa hiyo, ni fursa wana Temeke tunayo, wekezeni Temeke. Msiogope, serikali yenu ni sikivu na Rais Samia Suluhu Hassan anawapenda na anawaalika, karibuni sana kuwekeza katika nchi yetu," alisema Mapunda.

Elihuruma Mabelya, Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke, alisema dhamira ya serikali ni kuongeza kasi ya uwekezaji katika sekta zote.

Alitoa rai kwa wawekezaji kuwekeza katika sekta mbalimbali hususani maeneo ya kimkakati kama vile uwekezaji katika hoteli za kisasa, viwanda, makazi, viwanja vya michezo, bandari kavu na kilimo.

"Manispaa ya Temeke imesheheni fursa nyingi za kiuwekezaji na kiuchumi, tuna maeneo takribani 25 ambayo yanaweza kuchukuliwa kwa ajili ya uwekezaji kulingana na malengo ya manispaa.

"Hivyo, nitoe wito kwa wawekezaji kuwekeza Temeke na sisi kama manispaa tumejipanga vyema na tupo tayari kushirikiana katika kuimarisha kipato cha wawekezaji, uchumi wa halmashauri na nchi yetu kwa ujumla," alisema Mabelya.

Kongamano hilo lilifanyika katika ukumbi wa DYCC Chang'ombe likiambatana na uzinduzi wa Dawati la Uwekezaji kwa ajili ya kuratibu shughuli za uwekezaji.

Lilihudhuriwa na taasisi mbalimbali ikiwamo Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Mamlaka ya Mapato (TRA), Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na Benki ya DCB, pia TCCIA, NSSF na TPSF.






Nabii Mkuu wa Kanisa la Ngurumo ya Upako, Geor Davie na mkewe, wakiweka shada la maua kwenye kaburi la mtoto wao marehemu Nic Davie (Nisher) aliyekuwa mtayarishaji wa video mbalimbali za wanamuziki na filamu, mwimbaji na mtunzi wa nyimbo baada ya ibaada ya maziko, iliyofanyika nyumbani kwake Mji wa Daudi eneo la Kisongo, wilayani Arumeru, mkoani Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Bonite yazawadia washindi 27 shindano Coca-Cola VIP

**Na Mary Mosha,** MOSHI

KAMPUNI ya vinywaji baridi ya Bonite, imetoa sanduku 1,620 zenye thamani ya Sh.milioni 20 kwa washindi 27 kupitia shindano lake la Coca-Cola VIP Club lililofanyika katika viwanja wa kiwanda hicho, kilichoko Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro.

Lengo la kufanyika kwa shindano hilo ni sehemu ya kuwaongezea wateja wao na mitaji kuelekea msimu wa sikukuu za mwisho wa mwaka pamoja na kurudisha kidogo walichopata kwa jamii.

Akizungumzia shindano hilo, Meneja Mkuu wa Mauzo na Masoko, Christopher Loiruki, alisema shindano lilianza Oktoba 23, mwaka huu na kumalizika Desemba 9 na washiriki katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Singida walishindanishwa.

Alisema pia watatoa katoni nne hadi nane za soda kwa washiriki wote wa shindano hilo, kwa ajili ya kunywa katika maeneo yao ya biashara na nyumbani msimu wa sikukuu.

"Pia kwa wateja wetu tumekuwa na utaratibu wa kutoa elimu kwa wateja namna bora ya kufanya biashara, kuwaongezea vifaa ikiwamo viti, meza na majokofu kwa ajili ya kuhakikisha wateja wanakuwa kibiashara," alisema.

Akizungumzia shindano hilo, Loiruki alisema shindano hilo sio la mara ya kwanza ni utaratibu uliowekwa na kampuni hiyo, kuwasaidia wateja kujishindia zawadi mbalimbali ikiwa ni pamoja televisioni, gari na kuwaongezea mitaji kwa kuwapa masanduku ya soda.

"Tukizungumzia shindano hili, ilikuwa kila unaponunua soda za chupa ya kioo sanduku tano unapatiwa 'tiketi moja' mwisho wa shindano tiketi zote zinaingizwa kwenye droo ya bahati nasibu ambapo mshindi wa kwanza atajishindia zawadi ya sanduku 100 za soda, wapili sanduku 50 na watatu sanduku 30 katika kila mkoa wa biashara.

Alisema kila mkoa wa kibiashara wametoa sanduku 540 kwa washindi tisa ambayo ni mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na mikoa mingine ya kibiashara inayojumuisha Manyara na Singida.

Naye Mwakilishi wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania, Neema Tatock, alisema mashindano hayo ni halali huku akiwaondoa hofu wateja hao kuwa hakuna hitilafu zilizotokea katika mchezo kutokana na kufanyika kwa uwazi na ukweli.

"Washindi wamepatikana kwa njia ya haki na shindano lilikuwa likifanyika kwa uwazi na washiriki wote walishiriki na wakakubaliana na matokeo hivyo hakuna tatizo lolote lililojitokeza," alisema Neema.

Aidha, washindi wa shindano hilo, akiwamo Meneja wa Avila Bar, Aisha Rashidi, jijini Arusha eneo la Mihanzini, alisema ushindi huo utawasaidia wateja wao kupata huduma za uhakika.

# Watumishi wa umma kupimwa kwa tathmini ya kazi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, amesema matumizi ya mifumo ya PIPIMS, PEPMIS na HR Assessment katika utumishi wa umma nchini, inakwenda kufanya tathmini kwa watumishi serikalini pamoja na kuwabana ambao hawatekelezi majukumu yao.

Alisema hayo mwishoni mwa wiki jijini hapa wakati akizungumza na watumishi wa ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha.

Alisema serikali imedhamiria kuimarisha utumishi wa umma kwa kuhimiza uwajibikaji na kuhakikisha taifa linakuwa na utumishi unaopimika kwa muktadha wa kumpima mtumishi mmoja mmoja pamoja na taasisi zake kwa ujumla.

"Mfumo wa PEPMIS umekuja kuwa mbadala wa OPRAS, ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kuwa amelenga kuimarisha mifumo ya uwajibikaji inayowezesha viongozi na watumishi kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi kwa wakati na mahali popote, pia kuwabana wanaopenda kukaa ofisini bila kufanya kazi," alisema Naibu Waziri huyo.

Ridhiwani aliwataka maofisa utumishi na maofisa tawala kutembelea maeneo yote ya kazi ili kusikiliza changamoto zinaziwakabili watumishi walio chini yao na kutatua kero kwa wakati.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, amemshukuru Naibu waziri huyo kwa kufuatilia utoaji wa mafunzo unaoendelea katika mkoa huo na alisisitiza kuwa kutokana na kukua kwa teknolojia kwa zama hizi haihitaji watu wenye misuli badala yake wenye kuwajibika katika kazi.

Pia alisema mafunzo hayo yametolewa kwa wakati mwafaka kwa maofisa tawala, utumishi na rasilimali watu watabadilika na kuendana na teknolojia na kuachana na utaratibu wao wa utendaji kazi wa kizamani.

Vilevile, ameiomba Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, kuwanoa upya maofisa tawala, Utumishi na Rasilimali Watu wa mikoa na halmashauri kwa kuwa utendaji wao wa kazi sio wa kuridhisha kwa kuzingatia kuwa wamepewa jukumu la kuwasimamia watumishi wengine.

# Ataka elimu lishe itolewe kupunguza udumavu

**Na Allan Isack,** ARUSHA

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Arusha, Missaile Mussa, amewataka wajumbe wa Kamati ya Lishe mkoani humo, kuongeza wigo wa kutoa elimu ya lishe kwenye jamii ili kupunguza idadi ya watoto wenye udumavu maeneo ya vijijini katika mkoa huo.

Aliyasema hayo juzi wakati akifungua kikao cha Lishe Mkoa wa Arusha cha kuwasilisha taarifa za afua za lishe kwa kipindi cha robo ya kwanza kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mussa alisema, licha ya kuwapo kwa changamoto ya udumavu kwa watoto, lakini inaendelea kupungua siku hadi siku na kuwakumba hasa watoto wa maeneo ya vijijini inayochangiwa na uhaba wa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa lishe kwa watoto walio chini ya umri wa miaka miwili na miezi saba na kuwataka wataalam kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kupanua wigo wa kuwafikia wananchi hao.

"Bado mkoa wetu unakabiliwa na changamoto ya utukelezaji wa afua za lishe kutokana na sababu mbalimbali, hivyo niwatake wataalamu kuongeza wigo katika utoaji wa elimu kwa jamii na tufanye kazi kwa bidii ili kukabiliana na changamoto hii ya udumavu kwa watoto," alisema.

Alizitaka halmashauri zote za mkoa huo, kuipa kipaumbele ajenda ya lishe ikiwa ni pamoja na kupeleka fedha za kutekeleza afua za lishe kwa asilimia 100 kwenye maeneo yao kwa wakati kama inavyoelekezwa kwenye bajeti zao.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa afua za lishe kwa kipindi cha mwaka 2023/2024, Mratibu wa Lishe Mkoa wa Arusha, Doto Milembe, aliahidi kuendelea kupambana na udumavu kwa mpango mikakati wa kuendelea kutoa elimu hasa kwa wajawazito kupitia vikao mbalimbali, kliniki pamoja na mikutano inayoendeshwa kwenye ngazi ya jamii.

"Tunaendelea kuhamasisha kinamama na jamii kwa ujumla umuhimu wa ulaji wa makundi sita ya vyakula ili kupata virutubisho vinavyopaswa kwa watoto pamoja na kuongeza idadi ya milo kwa watoto hadi kufikia milo mitano inayoshauriwa kitaalamu," alisema.

Aidha, wadau walioshiriki kikao hicho, wameishukuru serikali kwa kuwa na mwamko wa kuhimiza umuhimu wa lishe kwa jamii na ushirikishwaji wa wadau jambo ambalo linarahisisha kuifikia jamii kwa pamoja kuliko kufanya kazi wenyewe.

Shekhe wa Wilaya ya Arusha, Hussein Said Ijunje, ambaye alimwakilisha Shekhe Mkuu wa Mkoa wa Arusha, alishauri kuongezwa nguvu zaidi kwenye suala hilo kwa ajili ya kuwafikia wananchi kwenye kata, vijiji na vitongoji na kushirikisha viongozi wa dini kwa kuwa wana ushawishi mkubwa kwenye jamii.





# El-Nino yasababisha hasara kwa wakulima wa pamba

**Na Waandishi Wetu**



Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude (kushoto), akikagua pembejeo za kilimo ikiwamo mbolea za kupandia na kukuzia mazao, ambazo zitagawiwa kwa wananchi 556 katika Kijiji cha Ngunga wilayani humo, ambao wamepitiwa na mradi wa umeme wa jua, ili wafanye kilimo chenye tija na kupata mavuno mengi. Kulia ni Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Dk. Sabinusi Chaula. **PICHA: SHABN NJIA**

WAKULIMA wa pamba kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa wametaja mvua ya El-Nino inayoendelea kunyesha nchini kuathiri kilimo hicho na kuwasababishia hasara kutokana na mashamba kujaa maji na kuharibu zao hilo linalohitaji mvua ya wastani.

Kwa mujibu wa mtafiti wa zao hilo kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Nchini (TARI) Ukiriguru, Dk. Paul Saidia pamba UKM 08 inayotumiwa na idadi kubwa ya wakulima inahitaji maji yasiyozidi milimita 500 tofauti na ilivyo kwa sasa maji yameongezeka zaidi.

Wakulima wanataja hali hiyo kushusha uzalishaji wa zao hilo kwa msimu ujao kutokana na mavuno kidogo yatakayopatikana kulinganisha na misimu mingine iliyokuwa na mvua za wastani.

Mkulima wa Kijiji cha Kitwechembogo wilayani Biharamulo, Charles Mbuga alisema, amelima ekari tatu kwa sasa ni eneo dogo ambalo lipo kwenye mwinuko ndilo lililobaki bila kuingiwa na maji ambapo analazimika kusubiri mvua ziishe ili apande upya.

"Matarajio kwa kipindi hiki ni madogo kwani ni tofauti na misimu mingine ambayo tulipata mavuno kutokana na mvua kuwa za wastani na zao hili haliitaji mvua nyingi kama za sasa," alisema Renatha Jackson, mkulima kutoka Kata ya Ruziba.

Mkulima wa kutoka Ibuka, Bundala Maziku alisema, mashamba ya pamba yamejaa maji na sasa wanaendelea kuweka matuta kando ya mashamba ili kuzuia maji kuingia ndani.

Alisema wana shaka ya kushindwa kulipa gharama za pembejeo ambazo walichukua kwa mkopo kwa ajili ya kuongeza uzalishaji.

Paul Mazinze kutoka Mwakalima wilayani Misungwi alisema, mvua imeifanya ardhi kutitia na muda wote inakuwa imejaa maji na kuwa majaruba jambo lililofanya washindwe kulima na kusubiri wakati mvua zitakapo koma.

Aliiomba serikali na wataalamu wa kilimo kuwatembelea ili kuwapa mbinu za kitaalamu ya nini wafanye kwa kuwa toka mvua ilipoanza hawajatembelewa na wataalamu na kuwafanya wasitishe shughuli hizo kwa muda hadi zitakapokata.

### AMCOS YAELEZA UKUBWA WA TATIZO

Hali hiyo imezua hofu pia kwa viongozi wa Vyama vya Msingi vya Kilimo na Masoko (AMCOS) kuhusu matarajio ya zao hilo kuadimika sokoni katika msimu ijayo huku wakiwahimiza wakulima kutokukata tamaa na mvua inapokata wapande tena.

Katibu wa AMCOS Kata ya Nyakahura Kahama, Emmanuel Paschal, alisema kwa msimu huu hawana mategemeo ya kufikia lengo kutokana na mvua.

Alisema katika msimu wa 2021/2022 walipata tani 59,000 kati ya tani 37,000 zilizokuwa zimelengwa katika makusanyo ya zao hilo, lakini kwa sasa hali ni tofauti na kulazimika kuwashawishi wakulima kurudia kupanda tena kwa mwezi Desemba mwishoni mwa Januari endapo mvua itapungua.

Mwenyekiti wa Chama cha Msingi Uyogo-Ushetu, Maganga Msanja, alisema, wana wakulima 275 na matarajio yao ni kupata tani zaidi ya 100 za zao hilo, mvua imesababisha kutofikisha.

Alisema mvua inaathiri ukuaji wa kilimo hicho na kuwataka wakulima kuzingatia maelekezo wanayopatiwa na wataalam ili kukabiliana na hali hiyo.

### WATAALAMU WAANIKA MBINU KUKINUSURU

Mtafiti wa zao hilo kutoka TARI Ukiriguru, Dk. Paul Saidia, anasema wakulima wanaweza kukabiliana na hali hiyo kwa kutumia njia mbalimbali ikiwamo kulima katika maeneo yasiyo ya bondeni.

"Wakulima ambao tayari wamepanda wahakikishe wanatengeneza mitaro itakayosaidia kuondoa maji shambani, walime kwa njia za matuta ili kuruhusu maji kupita katika maeneo ya wazi ili yasiathiri mazao yao," alisema Dk. Saidia.

Aidha, alisema kwa mbegu bora ya pamba ya UKM 08 inayokua kwa muda usiopungua miezi sita itastahimili kiwango cha maji ya milimita 500 pekee na ikizidi hapo zao hilo linaweza kuoza na ni muhimu kuchukua taadhari.

"Mbinu zote tumekuwa tukizipeleka kwenye Bodi ya Pamba ambayo kazi yake ni kuhakikisha zinawafikia wakulima na kuwasaidia kulima kwa tija," alisema Dk. Saidia.

Mkaguzi wa pamba kutoka Bodi ya Pamba (TCB), wilayani Kahama, Emmanuly Kireo, alikiri kuwapo kwa athari hizo na kusema kuwa mpaka sasa wameshindwa kujua ni hekari ngapi za mashamba zimelimwa na wakulima licha ya kuwa na marajio ya kupata tani 48,000.

Kireo alisema, wakulima wenye mashamba bondeni ndio wanaoathirika zaidi kulinganisha na wengine kwani maji yanapokuwa mengi shambani kama mashamba ya mpunga yanavyokuwa huwa pamba inashindwa kutoa maua yake.

Mkurugenzi Mkuu wa TCB, Marco Mtunga akizindua msimu wa ununuzi hivi karibuni alisema matarajio yao katika msimu wa ununuzi 2023/2024 ni kufikia uzalishaji wa tani 400,000 kulinganisha na uzalishaji wa tani 174,031 za msimu wa ununuzi 2022/2023.

Aidha, bodi hiyo inatarajia kuongeza mauzo kutoka dola za kimarekani milioni 227.1 hadi dola milioni 238.46 huku wakiwa na bajeti ya Shilingi bilioni tano kwa ajili ya umwagiliaji wa zao hilo.

### MIKAKATI YA WAKUU WA MIKOA

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, alitaja mikakati ya kunusuru pamba mkoani humo ikiwa ni pamoja na kusisitiza usimamizi wenye tija wa zao hilo utakaofanywa na maofisa ugani.

Alidokeza mpango wake wa kukutana na maofisa ugani wa ngazi zote kutoka wilaya zote kupeana mikakati ya kuwasaidia wakulima kulima kisasa na kukabiliana na athari za mvua hizo.

"Wiki ijayo nitakutana tuweke mikakati ili tuone namna ya kulifanya zao hili liwe na tija kiuchumi kwa mkulima na taifa kwa ujumla," alisema Makalla.

Alisema tayari serikali imeboresha kwa kiwango kikubwa sekta ya kilimo nchini na kwamba hakuna sababu ya uzalishaji wa zao hilo kukwama kwa aina yoyote wala kuzorota.

"Serikali imeweka mazingira rafiki kwa mkulima kwa kupunguzia gharama za pembejeo na kuboresha mbegu bora, hivyo ni wakati mwafaka kwa Mwanza kurudisha uzalishaji na kutoa Pamba itakayokidhi soko la kimataifa na itawezekana baada ya kupata ushauri kutoka kwa wataalamu," alisema Makalla.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme aliagiza maofisa ugani kuingia shambani wenyewe kukabiliana na tatizo hilo.

Aliwataka maofisa hao kuwatembelea wakulima na kuacha tabia ya kukaa ofisini ili kuwapatia elimu ya kilimo ambacho kinaendana na wastani wa mvua hizo.

"Serikali imetoa pikipiki 224 kwa Maofisa Ugani, hivyo hakuna kisingizio kwamba hamna usafiri lazima waende kwa wakulima wawapatie elimu ya Kilimo ambacho kinaendena na wastani wa Mvua sasa hivi," aliagiza Mndeme.

Alisema mazao yaliyoharibika siyo pamba pekee ni pamoja na mahindi kutokana na kuzidiwa mvua na serikali itahakikisha inakuwa karibu na wakulima ikiwa ni pamoja na kuwapa mbegu na elimu ya kuhimili mvua.

***Imeandaliwa na Shaban Njia (KAHAMA), Marco Maduhu (SHINYANGA), Restuta Damian (BIHARAMULO), Thomas Wandiba (SAUT), Vitus Audax (MWANZA).**

# Nipashe Spotika




MFUMO 5-4-1 UNAVYOWEZESHA USHINDI MCHEZO WA MTANDAONI eFOOTBALL UK. 12-13




# WACHEZAJI WA5 BORA EPL HADI SASA MSIMU HUU

**LONDON,** England

TUKO vizuri katika mambo mazito kuhusiana na msimu wa Ligi Kuu England, EPL, msimu huu wa 2023-24. Kampeni mpya ya Ligi Kuu England imekuwa ya kusisimua na kuburudisha kama kawaida na kutotabirika kabisa kumewafanya mashabiki wawe makini kwenye televisheni kila wiki ya mchezo hadi sasa.

Timu nyingine kama zilivyotarajiwa zimekuwa kwenye hali nzuri katika hatua za mwanzo za msimu mpya. Pia kumekuwa na mambo machache ya kustaajabisha huku baadhi ya wanasoka wakija kivyao katika muhula huu.

Wacha tuangalie wachezaji watano bora kwenye Ligi Kuu England hadi sasa msimu huu wa 2023-24.

**#5 Declan Rice (Arsenal)**

Jinsi mambo yalivyokwenda hadi sasa, Declan Rice anaonekana ana thamani ya kweli ya euro milioni 116. Katika siku zake za awali Arsenal, kiungo huyo wa zamani wa West Ham United ameonesha kwa nini anachukuliwa kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi kwenye Ligi Kuu England.

Rice amecheza vizuri na ameweka sauti kwa upande wake kwa kupiga pasi sahihi na uwezo wa kupanga kucheza kutoka kwa kina pamoja na kuvunja mashambulizi ya wapinzani. Rice pia amekuwa akifunga bao la muhimu mara kwa mara na amefurahisha kwa viwango vyake vya utimamu.

Anaweza kuwa tegemeo kwa 'Washikabunduki' hao msimu huu wanaopigania taji la Ligi Kuu.

**#4 Ollie Watkins (Aston Villa)**

Ollie Watkins amekuwa mchezaji aliyezaliwa upya chini ya Unai Emery. Aston Villa imekuwa moja ya timu zilizovutia zaidi kwenye Ligi Kuu msimu huu na kiwango chao nyumbani (ushindi mara 14 mfululizo) umekuwa wa kutia moyo sana.

Watkins amekuwa mtulivu, mwenye mwendo na uwezo wake wa kumalizia vizuri na sasa anachukuliwa kuwa mmoja wa washambuliaji bora wa kati katika Ligi Kuu ya England hivi sasa.

Katika mechi 15 kwenye ligi kuu England hadi sasa msimu huu, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, amefunga mabao nane na kutoa asisti sita.

**#3 Bukayo Saka (Arsenal)**

Arsenal wanapaswa kufanya kila lililo ndani ya uwezo wao kuhakikisha Bukayo Saka anacheza klabuni hapo kwa muda mrefu iwezekanavyo. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, ni mmoja wa mawinga bora zaidi kwenye sayari hii na anaendelea kutoa nguvu kwa kila mchezo.

Baada ya kuanza kampeni polepole, Saka amekuwa katika hali ya kuvutia hivi karibuni. Anapata njia ya kutengeneza nafasi za mabao katika takriban kila mechi anayocheza na pia ni hodari wa kutafuta mabao.

Uthabiti wa Saka umekuwa jambo muhimu, amefunga mabao matano na kutoa asisti sita katika mechi 14 za ligi hadi sasa msimu huu.

**#2 Erling Haaland (Manchester City)**

Erling Haaland alivunja rekodi kadhaa za mabao katika msimu wake wa kwanza pale Manchester City. Alifunga mabao 36 katika mechi 35 za ligi msimu uliopita, idadi kubwa zaidi ya mwanasoka yeyote katika msimu mmoja wa Ligi Kuu.

Anaonekana kuwa tayari kufikia rekodi hiyo au hata bora zaidi, jinsi mambo yanavyoenda. Haaland amefunga mabao 14 na kutoa asisti nne katika mechi 15 za Ligi Kuu hadi sasa msimu huu. Hawezi kuzuilika wakati yuko katika hali na harakati zake, msimamo na umaliziaji unaendelea kuwa wa kiwango cha dunia.

**#1 Mohamed Salah (Liverpool)**

Maoni yaliibuka wakati Liverpool ilipoamua kumpa Mohamed Salah mkataba mpya msimu wa majira ya joto wa 2022. Alikuwa ametimiza umri wa miaka 30 na licha ya kuwa tayari amepata hadhi kwenye Ligi Kuu, kulikuwa na wasiwasi juu ya muda gani angeweza kuendelea.

Salah ameondoa wasiwasi wote huo katika mwaka uliopita. Amekuwa katika kiwango kizuri sana kwa Liverpool msimu wa 2023-24. Sifa za kiufundi za nyota huyo wa Misri zinakamilishwa na akili ya mchezo na hii inamruhusu kuwa na matokeo chanya katika takriban kila mchezo anaocheza.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, amefunga mabao 10 na kutoa asisti sita katika mechi 15 za Ligi Kuu England hadi sasa msimu huu.

## ISIKUPITE

JEZI sita zilizovaliwa na Lionel Messi kwenye mechi wakati wa kampeni ya ushindi ya Argentina kwenye Kombe la Dunia la FIFA 2022 zimepigwa mnada kwa dola milioni 7.8 sawa na Sh. bilioni 19.6 za Tanzania.



# MFUMO 5-4-1 UNAVYOWEZESHA USHINDI MCHEZO WA MTANDAONI eFOOTBALL



**LONDON,** England

SOKA linaweza kuwa mchezo usiotabirika hata wakati makocha wanapojaribu wawezavyo kudhibiti matokeo. Kwa bahati nzuri, mchezo sasa unatazamwa na watu wengi zaidi kuliko hapo awali, ambapo inamaanisha kuwa akili nyingi sasa zinaweza kufikiria na kuboresha mbinu zilizopo kwenye mchezo.

**Katika makala haya, tutaangalia mfumo wa 5-4-1 na jinsi ya kutumia toleo lake la kipekee wakati wa kucheza eFootball 24 ya mtandaoni.**

Makala haya pia yatajumuisha miongozo ya uundaji na 'Maelekezo ya Mtu Binafsi' ambayo ni ya lazima kwa ubora zaidi wa matokeo.

Ingawa makala haya yametungwa kwa kuzingatia eFootball, mbinu zinazojadiliwa hapa zinaweza kutekelezwa karibu popote, ikiwa ni pamoja na michezo halisi ya soka.

Wale wanaofahamu vizuri mchezo wa eFootball wanajua kuwa kila nafasi ina uchanganuzi wa kipekee. Kwa mfano, kati ya fowadi wa kati, kuna 'jangili wa bao', 'mbweha kwenye Box' na 'Fowadi wa kina'.

Kwa hiyo, kuchagua aina sahihi ya kiungo au beki ni muhimu sana. Hebu sasa tuanze...

### USP ya 5-4-1 ni ni nini

Katika muundo wa kawaida wa 5-4-1, kuna upana mwingi unaozalishwa na 'mawinga' katika safu ya kiungo na ulinzi. Kwa kawaida kuna kiungo mshambuliaji wa kushoto na kiungo mshambuliaji wa kulia ambao mara nyingi huwaacha mabeki wa pembeni wa ulinzi, au beki wa kulia na kushoto kuingiliana.

Katika mfumo huu, hakutakuwa na mwingiliano kutoka kwenye mabawa. Hakuna kiungo wa pembeni, ni mabeki wa pembeni tu, ni mmoja tu ndiye atakayeruhusiwa kusonga mbele. Lengo ni kutetea nafasi za kati kwa idadi na kubatilisha mashambulizi ya upinzani kwa kuziba nafasi kwa nguvu.

Tumia mkakati huu kutetea bao la kuongoza dhidi ya wapinzani ukitumia kadi zenye nguvu au uitumie tu kukatisha tamaa na kubatilisha adui yako kwa mbinu bora ya kujilinda.

### Shambulio
### Wacha tuanze na mbele kwanza

Katika mfumo wa 5-4-1, huwa ni vema kwenda na mwindaji bao, hasa mtu mwenye kasi ya juu. Lakini katika toleo langu la 5-4-1, hii inakuwa isiyoweza kujadiliwa. Mshambuliaji lazima awe na kasi, hata ikiwa ni sifa yake pekee aliyonayo.

Michael Owen ni mmoja wa washambuliaji wenye kasi zaidi katika mchezo huo. Akiwa jangili wa goli, atafanya mbio za moja kwa moja kwenye goli, lakini hawezi kuupiga mpira kwa kichwa.

Sababu ni kwamba katika toleo langu la 5-4-1, hakuna mawinga kwenye kiungo. Mabeki wa pembeni hushikamana na majukumu ya ulinzi na hawasaidii katika mashambulizi.

Kwa hiyo, hakutakuwa na mawinga ambao wanaweza kusambaza mpira kutoka kwenye mabawa. Kwa hiyo, chagua mshambuliaji mwenye kasi ya juu kama vile Owen au Kylian Mbappe. Wachezaji hawa ni wafungaji wazuri na wenye kasi ya ajabu, hata kama hawana uwezo wa kupiga vichwa.

Mbali na kuwa na kasi, jangili au mwindaji haramu wa mabao kila mara hutoboa mbio za moja kwa moja ili kuingia nyuma ya safu ya ulinzi, tofauti na washambuliaji wa aina nyingine.

### Kiungo

Kwa kawaida, katika jadi ya 5-4-1, kuna viungo wawili wa upana. Lakini upekee wa mfumo huu ni kwamba kuna wachezaji wanne wa ulinzi, au wachezaji wanne waliowekwa kama viungo wakabaji.

Inamaanisha tu kwamba hakuna hata mmoja wa wachezaji hao atakayekuwa pembeni. Lengo ni kuwafanya wachezaji hawa kujipanga kihalisi kama ukuta ili kukinga safu ya nyuma.

Muundo wa timu wakati wa kushambulia: kumbuka jinsi viungo wakabaji wawili wakijipanga kwa kina. Unaweza kuona Gilberto Silva na Fabinho ni viungo wawili wa aina hiyo, kumaanisha kuwa wanabaki nyuma na kuzingatia majukumu yao ya ulinzi.

Baadaye tuna Patrick Vieira ambaye ndiye 'mwangamizi', kumaanisha kwamba hatakuwa na kina kirefu kama wale watu wawili watia nanga. Atatoa kiwango cha uhamaji wa juu, hata wakati unachezwa kama kiungo mkabaji tofauti na kiungo mshambuliaji.

Mchezaji mwingine lazima awe 'Box-to-Box', hasa mtu mwenye sifa nzuri za kushinda mpira. Ninayempenda zaidi hapa ni mtu kama Douglas Luiz, mchezaji ambaye ni imara katika ulinzi na ana ujuzi mzuri wa kucheza mpira.

Mchezaji kama huyo ni muhimu, kwani waharibifu na watu wanaotia nanga wana ujuzi wa kumiliki mpira. Kwa hvyo, hatupaswi kushawishika kuchezesha viungo wote wanne katika mfumo huu.

Viungo wa Box-to- Box ni mchanganyiko mzuri wa nguvu, uwezo wa kulinda na ustadi wa mpira. Kiungo bora wa jumla wa box-to-box katika eFootball 24 ni Jude Bellingham.

### Ulinzi

Katika ulinzi, ni bora kuwa na beki wa kati akishirikiana na mabeki wengine wawili. Nimemchagua Marquinhos kama beki wa kati pamoja na Virgil van Dijk na mwanafunzi wake, Mathijs de Ligt.

Kama mabeki wa pembeni, lazima kuwe na 'Beki Kamili' mmoja na 'Mmaliziaji kamili'. Mantiki ni kwamba hata kama beki huyo wa pembeni atapanda kumuunga mkono mshambuliaji pekee, bado kutakuwa na safu ya watu wanne huku beki wa kulia mwenye akili ya ulinzi akisaidiana na mabeki watatu wa kati.

Wakati wa awamu ya kushambulia ya mchezo, ona jinsi beki wa kushoto Raphael Guerrero anavyosukuma juu ili kuanzisha mashambulizi. Pia, safu ya ulinzi bado imechafuka, ikifunikwa na Wan-Bissaka mwenye nia ya kujihami.

Unahitaji mchezaji kama 'njia ya kupita' baada ya kumiliki mpira. Beki wa pembeni anayeshambulia au hata mlinzi wa pembeni anaweza kuwa mbeba mpira. Mlinzi bora katika mchezo huo ni Aaron Wan-Bissaka.

Mtindo wa uchezaji wa timu lazima uwe wa kukabiliana na mipira mirefu. Chagua kocha aliye na uwezo wa juu kama Cristo Valbuena mwenye ustadi wa kucheza wa timu 85. Unaweza hata kumchagua Jose Mourinho, ambaye ana ustadi wa kucheza wa timu 82.

Katika mfumo wa kushambulia kwa mipira mirefu, timu hulinda kutoka chini kwenda juu na kuunda ukuta wa asili wa ulinzi karibu na eneo la hatari. Inafanya mfumo kuwa bora kwa uundaji wa 5-4-1.

Mshambuliaji anaweza kupewa maelekezo ya mtu binafsi ili hata yeye ashuke kusaidia katika ulinzi.

Hiyo inafanya kuwa mfumo wa mwisho kabisa wa ulinzi katika mchezo. Katika hatua za baadaye za mchezo wa mtandaoni, hasa ikiwa una kiongozi, jaribu mfumo huu na uhisi mpinzani wako akilia kwa kufadhaika.

### Faida na hasara

Huu sio mfumo rahisi kutekeleza, hata na mabeki wote. Kumbuka kwamba kwa sababu una mabeki wengi kwenye timu yako, bado huwezi kupenyeka. Bado unaweza kukubali kutoka kwa pembe.

Kusudi ni kutoruhusu mpinzani wako afunge bao, hata kama hiyo inamaanisha kutojifunga mwenyewe. Mfumo huu ni bora zaidi dhidi ya wapinzani wa 'Lipa ili Ushinde' ambao wana kadi zote za Epic na kadi za 'Big Time', ambazo baadhi yake zimeoneshwa katika mifano katika makala haya.

Ubaya mkubwa ni kwamba mpinzani wako atakuwa na mpira mwingi, kama ilivyo kwa timu yoyote inayotaka kulinda kwa namba. Ni lazima uwe tayari kiakili ili kufunga nafasi kwa vipindi vikubwa vya mchezo.

Mpinzani atajituma namba zaidi mbele kwa nia ya kufunga, na kuwafanya wawe rahisi kushambuliwa na mashambulizi ya kaunta. Ukiwa na pasi moja tu iliyopangwa kwa wakati ipasavyo, mshambuliaji wako pekee anaweza kutumia kasi yake na kujikuta akiwa dhidi ya mmoja na kipa wa timu pinzani.

Kwa kifupi, unapolinda mabao mawili au hata bao moja, mfumo huu unakuhakikishia ushindi.

KYLIAN MBAPPE

## Nukuu

"Si bahati mbaya, inastahili. Tulitoa pointi mbili lakini ukiruhusu penalti, unastahili. Kama ilivyokuwa katika mechi dhidi ya Tottenham [iliyomaliza kwa sare ya 3-3] na Liverpool [wakati City ilipotoka sare ya 1-1], tulikuwa bora, lakini, tena hatuna uwezo wa kushinda," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola, baada ya sare ya mabao 2-2 juzi, Jumamosi dhidi ya Crystal Palace.**



"Athari yake katika mchezo, anachofanya. Namjua Declan Rice amekuwa akifunga mabao, Saliba akiwa nyuma, kama vile Odegaard alivyokuwa mwaka jana... kwangu mimi, mwaka huu, Bukayo Saka ni vile ninavyoweza kusema hivi kwani ni juhudi kubwa ya timu - anabeba timu mabegani mwake," **Straika wa zamani wa Arsenal na Ufaransa, Thierry Henry.**




"Habari za uongo: Kikosi bora cha JM [Jose Mourinho]. Habari za uongo. Sijawahi kufanya hivyo. Siku zote nilikataa kufanya hivyo, haitatokea kwangu kuifanya hivyo. Nimekuwa na wachezaji wengi wa daraja la juu, lakini la muhimu zaidi ni kile wachezaji hao wananipa. Wachezaji ambao walinipa kila kitu: ubora, juhudi, damu na roho, wote wako kwenye kumi na moja yangu bora. Wote. Ndiyo maana siku zote nilikataa kuchagua kikosi changu bora. Nawapenda wachezaji wangu, nawaheshimu wachezaji wangu. Habari za uongo... Tafadhali heshimu historia yangu na uwaheshimu wavulana wangu," **Jose Mourinho akikana hajawahi kutaja kikosi chake bora**



# MAMBO 10 USIYOYAJUA, SIMBA, YANGA ZIKIREJEA TENA LIGI KUU BARA



Kiungo mshambuliaji wa Simba, Saido Ntibazonkiza, ni mchezaji anayeongoza kwa kufunga mabao mengi ya penalti kwenye Ligi Kuu mpaka sasa, akifanya hivyo mara mbili, katika mechi dhidi ya Prisons na juzi dhidi ya Kagera Sugar.

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE mwishoni mwa wiki Simba na Yanga, zilirejea tena Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kukosekana kwa takriban mwezi mzima zikiwa kwenye pilikapilika za mechi hatua ya makundi, Ligi ya Mabingwa Afrika.

**Simba ambayo mara ya mwisho ilicheza mechi yake Novemba 9, mwaka huu dhidi ya Namungo kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam na kutoka sare ya bao 1-1, Ijumaa ilishuka uwanjani hapo kucheza dhidi ya Kagera Sugar na kupata ushindi wa mabao 3-0, yaliyowekwa wavuni na Saido Ntibazonkiza, Sadio Kanoute na nahodha, John Bocco.**

Jumamosi, kwenye Uwanja wa Azam Complex, Yanga nao walishuka dimbani kwa mara ya kwanza tangu Novemba 8, mwaka huu ilipocheza dhidi ya Coastal Union katika Uwanja wa Mkwakwani, Tanga na kushinda bao 1-0, na kucheza dhidi ya Mtibwa Sugar, ikipata ushindi wa mabao 4-1.

Kwa mechi hizo mbili tu, tayari kuna rekodi na takwimu kwa timu na wachezaji zimewekwa na kubadilika kwenye ligi hiyo.

Zifuatazo ni baadhi ya takwimu na rekodi mbalimbali za kuvutia kwenye Ligi Kuu ambayo kwa sasa ipo katika raundi ya 13.

### 1. Simba, Namungo vinara wa penalti

Timu za Simba na Namungo ndizo zilizobahatika kupata penalti nyingi mpaka sasa kwenye Ligi Kuu, kila mmoja akipata tatu.

Baada ya kupata penalti Ijumaa katika mechi dhidi ya Kagera Sugar ikiwekwa wavuni na Saido, Simba kwa sasa imefikisha penalti tatu huku zote zikiwa zimeweka kwenye kamba.

Namungo nayo imebahatika kupata penalti tatu, lakini yenyewe ikikosa moja na kupata mbili ambazo zilifungwa na Derrick Mukombozi na Fabrice Ngoyi, huku Mukombozi akikosa moja.

### 2. Saido aongoza mabao ya penalti

Kiungo mshambuliaji wa Simba, Saido anaongoza mpaka sasa kwa kufunga mabao ya penalti, akifanya hivyo mara mbili kati ya penalti tatu ambazo timu yake imebahatika kuzipata.

Ijumaa iliyopita alifunga penalti yake ya pili, ya kwanza ilikuwa ni Oktoba 5, Uwanja wa Sokoine Mbeya, timu yake ilipocheza dhidi ya Prisons na kushinda mabao 3-1.

Penalti moja ya Simba ilifungwa na Jean Baleke, Septemba 21, mwaka huu, Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam dhidi ya Coastal Union, iliposhinda mabao 3-0.

### 3. Yanga, Azam zaongoza kwa ushindi

Vinara wa Ligi Kuu mpaka sasa, Azam FC na Yanga zinaongoza kwa kushinda mechi nyingi kuliko zingine mpaka sasa. Ushindi wa mabao 4-1 ilioupata Yanga juzi dhidi ya Mtibwa Sugar umekuwa ni wa tisa mpaka sasa sawa na Azam FC.

Wakati timu zote zikishinda mara tisa, Yanga imecheza mechi mbili pungufu ya Azam, ikiwa imeshuka dimbani mara 10, dhidi ya mara 12 ambazo Wanalambalamba wamecheza.

### 4. Yanga haijatoka sare hadi leo

Yanga ndiyo timu pekee kwenye Ligi Kuu ambayo haijatoka sare yoyote mpaka sasa. Timu hiyo imecheza mechi 10, ikishinda tisa na kupoteza moja tu ilipofungwa mabao 2-1 dhidi ya Ihefu FC, Oktoba 4, mwaka huu kwenye Uwanja wa Highland Estates, Mbarali, Mbeya.

### 5. Tabora United sare za kumwaga

Timu ya Tabora United inaongoza kuwa na sare nyingi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Ina sare sita mpaka sasa zikiwa ni nyingi zaidi kuliko timu yoyote mpaka kufikia raundi ya 13.

Imecheza mechi 12, imeshinda michezo mitatu na kupoteza idadi kama hiyo.

### 6. Mtibwa Sugar kapu la mabao

Kipigo cha mabao 4-1 ilichokipata juzi dhidi ya Yanga, Mtibwa Sugar inakuwa ni timu inayoongoza kwa kuruhusu mabao mengi kwenye ligi mpaka sasa. Imeruhusu wavu wake kuguswa mara 28 ambayo ni idadi ya juu zaidi kwa timu moja kuruhusu kwenye ligi hadi sasa.

### 7. Azam inafunga kwa swaga

Azam ndiyo timu inayoongoza kwa kufunga mabao mengi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa.

Tayari timu hiyo imeshaweka wavuni mipira mara 31, ikifuatiwa na Yanga ambayo imeshafikisha jumla ya mabao 30 ya kufunga.

### 8. Yanga ukuta wa chuma

Yanga imeruhusu mabao sita tu katika wavu wake mpaka sasa kwenye ligi, ikiwa ni idadi ya chini zaidi. Azam inafuatia ikiwa imeruhusu wavu wake kuguswa mara 10 na Simba ya tatu ikiwa imeruhusu mara 11.

### 9. Simba, Yanga zapoteza moja tu

Simba na Yanga zimepoteza mechi moja tu mpaka sasa zikiwa ndiyo timu zilizopoteza chache zaidi, kwani hakuna ambayo haijapoteza mechi. Wakati Yanga ikipoteza mechi yake dhidi ya Ihefu kwa mabao 2-1, Simba ilifungwa dhidi ya Yanga mabao 5-1, mechi iliyochezwa, Novemba 5 mwaka huu.

### 10. Mtibwa imeshinda moja tu

Mtibwa Sugar imeshinda mechi moja tu mpaka sasa ikiwa ni timu iliyoshinda mechi chache zaidi.

Licha ya kuburuza mkia ikiwa na pointi tano kwa michezo 13 iliyocheza, lakini pia imeshinda mechi moja tu iliyopita Oktoba 26, mwaka huu kwa kuifunga Geita Gold.

**JE, WAJUA?**



MABAO mawili aliyofunga Stephane Aziz Ki dhidi ya Mtibwa Sugar juzi wakati Yanga ikishinda 4-0, yanamfanya kuwa kinara wa ufungaji hadi sasa Ligi Kuu Bara baada ya kufikisha tisa, akifuatiwa na Jean Baleke (Simba) aliyefumania nyavu mara saba sawa na Maxi Nzengeli (Yanga) na Feisal Salum 'Fei Toto' (Azam FC).



## HABARI DODOMA

# VETA yatakiwa mafunzo yanayokidhi soko la ajira

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira, Vijana na Wenye ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, ameitaka Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini (VETA) kupanga na kutekeleza mikakati mbalimbali ili kutoa elimu na mafunzo yanayokidhi mahitaji ya soko la ajira.

Prof. Ndalichako alisema hayo juzi alipokuwa akitoa hotuba kwenye mahafali ya chuo hicho Kanda ya Kati yalijumuisha wahitimu wa kozi mbalimbali.

"Endeleeni kuboresha miundombinu na vifaa vya kufundishia ili kuwawezesha vijana wetu kupata elimu na ujuzi unaokidhi viwango vya kimataifa.

Alisema ni faraja kuona vijana wengi wanaendelea kupata ujuzi mahsusi unaowawezesha kupata ajira au kujiajiri wenyewe. "Hali hii itasaidia katika kuinua uchumi wao pamoja na taifa mafunzo ya ufundi ni eneo la kipaumbele kikubwa sana kwa serikali yetu," alisema.

Pia aliwataka wahitimu wote waliopata mafunzo ya ujuzi mbalimbali kwenda kuyafanyia kazi ili kujikwamua kichumi kwa kujiajiri wenyewe.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa VETA, Dk. Prosper Mgaya, alisema kutokana na ushindani katika soko la ajira ndani na nje ya nchi, ameanza mikakati ya kutoa mafunzo na vyeti ambavyo vitawasaidia wahitimu kutoa ushindani kwenye soko la ajira.

"Hivi sasa tupo katika mchakato wa kuanza kutoa mafunzo na vyeti ambavyo vitawawezesha wahitimu wetu kupata ajira nje ya nchi ili kutoa ushindani kwa mataifa mengine wakiwamo mjirani zetu Wakenya na mataifa mengine," alisema.

Alisema ili kufanikisha wameshapeleka wakufunzi nchini Afrika Kusini kujifunza kuendesha mafunzo hayo na kutoa vyeti vyenye hadhi ya kimataifa ili kuwezesha wahitimu kupata ajira nchi za nje.

Alisema katika mchakato wa mabadiliko ya mitaala ya elimu unaoendelea hivi sasa wamepewa jukumu na serikali la kuandaa mitaala ya ujuzi na vitabu.

"Tunaishukuru serikali kwa kutuwezesha fungu la kutosha ili kukamilisha kazi ambayo tunatarajia hadi ifikapo Januari mwakani mitaala hiyo pamoja na vitabu vitakuwa tayari kwa ajili ya kuanza kutumika," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, akishirikiana na wananchi wa kata za Miyuji na Mnadani jijini humo kufanya usafi wa mazingira kwenye mfereji unaopitisha maji ulioko pembezoni mwa barabara ya Dodoma na Arusha, Maili Mbili jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# RC apiga marufuku abiria kutupa taka ovyo barabarani

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amepiga marufuku abiria wanaotumia mabasi kutupa taka ovyo pembezoni mwa barabara na watakaobainika watakamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Alisema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Mnadani na Miyuji Jiji la hapa, baada ya kumalizika kufanya usafi wa mazingira kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali zinazojihusisha masuala ya usafi wa mazingira.

Alisema kuwa Dodoma ni makao makuu ya nchi ni lazima watu wote wazingatie usafi wa hali ya juu. "Naizingatiwe kuwa hapa tunapokea wageni mbalimbali wanaoingia kutoka mikoani mbalimbali hivyo ni vyema kujenga utamaduni wa kupenda usafi wa mara kwa mara.

"Hivyo niwatake waendesha vyombo vya usafiri vya moto kwa maana mabasi na wengineo tujihadhari na utupaji wa taka pembezoni mwa barabara zote kwa ajili ya kujilinda na afya," alisema.

Aliwataka waendesha magari wote na abiria wanaoingia mkoani hapa, kuwa wasafi.

"Kwani na sisi hatupendi uchafu huo na hatutakaa kimya watakaobainika tutalazimika kuwaburuza mahakamani," alisisitiza. Aliwataka wakazi wa kata hizo kujenga utamaduni wa kupenda kufanya usafi bila kulazimishwa ili kuepuka kutozwa faini.

Mkuu wa Kitengo cha Usafi na Mazingira Jiji la Dodoma, Dickson Kimaro, alisema jiji litaendelea kuhimiza suala la usafi wa mazingira na kuwachukulia hatua kali za kisheria watakao kaidi.

Alisema hakuna mtu atakayefumbiwa macho atakapokiuka taratibu za ufanyaji wa usafi kwa kuwa Jiji la Dodoma ni sura ya nchi na wageni wengi wanaingia na kutoka.

"Kila mwananchi katika eneo lake ni lazima afanye usafi na usafi iwe tabia ya mtu kuanzia nyumbani kwake na liwe somo hata kwa watoto waliopo ndani ya familia bila kusubiri kusukumwa au kuchukuliwa hatua za kisheria," alisema Kimaro.

# Benjamin Mkapa yapokea kesi 100 ukatili kijinsia

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

HOSPITALI ya Benjamin Mkapa imepokea kesi zaidi ya 100 za ukatili wa kijinsia kutoka maeneo mbalimbali.

Mkurugenzi Msaidizi wa Utafiti na Ubunifu, Hindu Ibrahim, alisema hayo jana wakati wakiadhimisha siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia.

Alisema wamekuwa wakipokea kesi hizo na kuzifanyia kazi ikiwemo kutoa maelekezo kwa jamii ili kujikinga na ukatili wa kijinsia katika maeneo mbalimbali.

"Kesi ni nyingi sana za ukatili wa kijinsia hivyo BMH tunaendelea kutoa elimu kwa jamii ili kuhakikisha wanautokomeza ukatili wa kijinsia kwa jamii," alisema Hindu.

Alifafanua zaidi ya kuwa lengo lao ni kuona ukatili unatokomezwa kwa jamii ili watoto waweze kutimiza ndoto zao za hapo baadaye.

Alifafanua zaidi ya kuwa wanatarajia kupitia katika vyuo vikuu kwa ajili ya kutoa elimu kuhusu suala zima la kupinga ukatili wa kijinsia.

Alisema wamegawanyika katika makundi mbalimbali ili kuhakikisha wanapiga hatua kupinga ukatili wa kijinsia kwa watoto na wanawake.

Mkazi wa Jiji la Dodoma, Zainabu Kibena, aliomba serikali izidi kuweka jitihada kutokomeza ukatili.

Kibena alisema ukatili wa kijinsia unarudisha nyuma maendeleo kwa wananchi na kwamba jitihada zinatakiwa kutokomeza.

Alisema matukio ya ukatili ni mengi kwenye jamii ni vyema yapigwe vita ili yatokomezwa nchini.

Aidha, alisema wanapaswa kuendelea kutoa elimu kwa jamii ili waweze kutambua masuala ya ukatili wa kijinsia kwa watoto na wanawake hayakubaliki katika jamii.

Hospitali ya Benjamin Mkapa imekuwa ikitoa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya kupinga ukatili wa kijinsia mijini na vijijini na hii yote ni kutaka kutokomeza kabisa ukatili wa kijinsia.



## CCM yaagiza mifumo kifedha yenye tatizo itatuliwe

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

KAMATI ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe, imeiagiza serikali kutatua haraka matatizo ya mifumo ya kifedha ili kukamilisha miradi ya serikali iliyokwama kwa muda mrefu na wananchi kuendelea kupata huduma.

Agizo hilo lilitolewa na Mjumbe Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa mkoani Njombe (MNEC), Daniel Okoka, wakati wa ziara ya utekelezaji wa ilani katika ujenzi wa bweni la wavulana Shule ya Sekondari Utalingoro Halmashauri ya Mji Njombe.

Okoka alisema suala la mfumo kukwama mara kwa mara unasababisha kufifisha ufanisi kwa miradi mingi ya serikali na kueleza hofu yake juu ya shule za msingi na sekondari ambazo hazijakamilika na zinapaswa kuanza kupokea watoto kuanzia Januari mwaka 2024.

"Suala la changamoto ya mfumo sisi kama chama kwa kweli tunasikitishwa na tunaona jambo hili halitendi haki kwa sababu kinachotokea sasa ni kukwamisha malengo tuliyoyakusudia na hizi ni dalili za kwamba itakapofika mwezi wa kwanza tunapotakiwa kupokea wanafunzi tutapata shida ya miundombinu," alisema Okoka.

"Kila siku mfumo sasa tunaiagiza serikali iondoe changamoto hii haraka iwezekanavyo ili miradi hii ikamilike kwa wakati na inakusudia nia njema aliyonayo Rais ikamilike, iondoe kero ambayo wananchi wanaipata," alisema.

Awali Mratibu wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) Halmashauri ya Mji Njombe, Mariam Monjesa, alisema mradi huo unasuasua kwa sababu ya changamoto ya mfumo.

"Tumekuwa tukidaiwa na mafundi, wazabuni, lakini kama changamoto ya mfumo itatatuliwa kwa wakati naamini kwamba kazi zetu zitakamilika haraka ili kuendelea kutoa huduma zilizokusudiwa," alisema Monjesa.

Diwani wa Kata ya Utalingoro, Erasto Mpete, alisema mradi huo uliibuliwa na wananchi kutokana na upungufu katika shule hiyo.

# Ukosefu elimu matumizi viuatilifu waathiri uzalishaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ASILIMIA 75 ya wakulima nchini wanakosa elimu sahihi ya matumizi ya viuatilifu na visumbufu vya mimea kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo uhaba wa wataalamu na kupunguza tija kwenye uzalishaji.

Inadaiwa kuwa wakulima hao huwa wanapata elimu hiyo kutoka kwa wafanyabiashara wa maduka ya viuatilifu au kwa wakulima wenzao hali inayosababisha upotoshaji.

Serikali kupitia Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu (TPHPA), imeanza kuwaelimisha wafanyabiashara wa viuatilifu kutoka katika mikoa 10 nchini kuhusu matumizi sahihi ya viuatilifu hivyo ili kukidhi matakwa ya sheria.

Mafunzo hayo yalianza kufanyika jijini hapa na mikoa ambayo wafanyabiashara wake wanashiriki ni Mbeya, Iringa, Ruvuma, Njombe, Songwe, Rukwa, Katavi, Arusha, Morogoro na Dodoma.

Meneja wa TPHPA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Emmanuel Mausa, alisema baadhi ya wafanyabiashara wanawapatia wakulima maelezo ya viuatilifu hivyo ambayo siyo sahihi.

Alisema hali hiyo imekuwa ikisababisha viuatilifu hivyo kutofanya kazi inayokusudiwa na kuwasababishia wakulima tija ndogo kwenye uzalishaji.

"Ni asilimia ndogo sana ya wakulima huwa wanapata elimu kutoka kwa maofisa ugani, kwa hiyo tumeamua tuwajengee uwezo wafanyabiashara hawa ili wawe na uelewa wa kutosha kutoa elimu kwa wakulima wetu," alisema Mausa. Mratibu wa mafunzo hayo, Jumanne Musalama, alisema kwa mujibu wa sheria namba nne ya afya ya mimea ya mwaka 2020 ibara ya 37, inataka kila mtu anayejishughulisha na viuatilifu kupata mafunzo.

Alisema wafanyabiashara wa viuatilifu ni kundi muhimu kwenye usambazaji wa elimu kwa wakulima na kuwataka kuwapatia wakulima maelezo sahihi. Alisema kila mfanyabiashara anayeuza viuatilifu ni lazima apate mafunzo maalumu ili kukidhi matakwa ya sheria na kwamba baadaye utapitishwa msako maalumu ili kuwabaini wanaokiuka sheria hiyo.

Alisema kila mfanyabiashara wa viuatilifu ni lazima asajiliwe na kupatiwa cheti ili kuthibitisha amepata mafunzo na watakuwa wanawatembelea mara kwa mara ili kuwakumbusha. "Kwa hiyo elimu hii itakuwa endelevu ili kuhakikisha kila mmoja anayetekeleza sheria iliyoanzisha mamlaka hii, tunaamini baada ya kuwaelimisha wafanyabiashara hawa wataongeza ujuzi kuwaelimisha wakulima," alisema Musalama. Baadhi ya wafanyabiashara walioshiriki mafunzo hayo walisema yatawasaidia kuaminiwa zaidi na wakulima pamoja na kufanya kazi yao kwa uhakika.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Teodonsia Mwolo, alisema mafunzo hayo pia yanawasaidia kuelewa namna ya kudhibiti matumizi ya viuatilifu hiyo ili kuepusha madhaya ya kiafya na kimazingira.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Mbeya, Samora Mshang'a, alishauri wakulima wote nchini kupata mafunzo hayo ili wavitumie kwa kuzingatia sheria na kuepuka madhara.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, akitoa maelekezo kwa Mhandisi wa Halmashauri ya Busokelo, Wilaya ya Rungwe kuhusu kukamilisha vyumba vya madarasa katika Shule ya Sekondari Lupata ili wanafunzi waanze masomo Januari bila usumbufu. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Operesheni ukaguzi magari yazuia matano kusafiri

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Mkoa wa Mbeya, limeanzisha operesheni maalumu ya ukaguzi wa mifumo ya magari ya abiria yanayofanya safari zake kati ya mkoa huo na mingine ili kupunguza ajali zinazotokana na ubovu wa mifumo hiyo.

Operesheni hiyo ya kushtukiza ilianza kufanyika juzi katika kituo kikuu cha mabasi ya masafa marefu cha Mkoa wa Mbeya na wakaguzi wa jeshi hilo chini ya Mkuu wa Kikosi, Mrakibu wa Polisi Hussein Gawile walianza kukagua mabasi hayo kabla hayajaanza safari.

Katika operesheni hiyo mabasi matano yalizuiliwa kuanza safari mapema baada ya kubainika kuwa yalikuwa na hitilafu kwenye mifumo ikiwamo ya breki ambayo ilikuwa inahatarisha usalama wa abiria.

Wasimamizi wa mabasi hayo na wamiliki walitakiwa kuyarekebisha kwanza mabasi hayo kabla ya kuendelea na safari kwa lengo la kulinda usalama wa abiria na mali zao.

Mrakibu Gawile alisema walikagua mabasi 45 ya masafa marefu na matano pekee ndiyo yalibainika kuwa na kasoro na walisimamia urekebishaji wake mpaka ulipokamilika ndipo wakaruhusiwa kuondoka.

"Lakini tunazungumza na abiria wa mabasi kuhusu hatua wanazopaswa kuzichukua wanapobaini kitendo chochote kibaya wawapo safarini, tunawaelimisha kuhusu kampeni ya abiria paza sauti ambayo inawahamasisha abiria kutoa taarifa," alisema Mrakibu Gawile.

Mwenyekiti wa Mabalozi wa Usalama Barabarani (RSA), Mkoa wa Mbeya, Furaha Malele, aliwasihi madereva wa vyombo vya moto kufanya kazi kwa kuzingatia sheria za usalama ili kuepuka ajali.

Aliliomba Jeshi la Polisi kuendelea kusimamia sheria kwa kuhakikisha madereva wote wana leseni za kufanyia kazi hiyo na wamepata mafunzo yanayostahili.

Malele alisema ajali nyingi zinasababishwa na uzembe wa madereva pamoja na watumiaji wengine wa barabara.

"Mtu anapopatiwa leseni ya udereva tafsiri yake ni kwamba amefuzu mafunzo, sasa tunaomba sheria ziendelee kuzingatiwa ili kulinda maisha ya wananchi pamoja na usalama wa vyombo," alisema Malele.

Ofisa Leseni wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Nuru Mwakajumilo, aliwataka abiria wote wanaposafiri kupatiwa tiketi zinazoonyesha nauli halisi wanazotozwa.

Aliwataka abiria kuzitunza tiketi hizo ili ziwasaidie wanapopata matatizo ikiwamo kupotelewa na mizigo kwenye basi husika na kuwataka kuwa na tiketi za kidijitali.

Baadhi ya abiria walilishukuru Jeshi la Polisi kwa kuanzisha operesheni hiyo kuwa itawasaidia kuwa salama wakati wa safari zao hasa katika kipindi hiki cha mwisho wa mwaka ambacho abiria ni wengi.

Mmoja wa abiria hao, Stanleya Kapinga alisema kitendo cha maofisa wa Jeshi la Polisi kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kitasaidia wamiliki wa mabasi kuwa makini na kuepusha ajali.

Alisema hakuna mmiliki wa basi ambaye anapenda gari lake lizuiwe kufanya kazi kwa maelezo kuwa vyombo hivyo ndivyo vinawaingizia kipato.



# Masheha watakiwa kusimamia nyumba za shirika

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mkuu wa Shirika la Nyumba Zanzibar, Mwanaisha Ali Said, amewataka masheha kuendeleza ushirikiano ili kuzikabili changamoto zinazojitokeza katika nyumba za maendeleo ya shirika hilo.

Aliyasema hayo jana katika Shirika la Nyumba, Darajani Unguja wakati wa kikao cha majadiliano na masheha wa shehia ambao zina nyumba za shirika hilo.

Alisema changamoto hizo huharibu taswira ya awali na kuondoa uhalisia.

Aidha, alisema masheha wa shehia ni wadau wakubwa katika shirika ambao pia ni mashuhuda wa changamoto zote zinazojitokeza katika nyumba hizo yakiwamo matumizi yasiyo sahihi katika nyumba hizo.

Aidha, alisema mikakati ya pamoja inahitajika ili kuhakikisha wanadhibiti vitendo viovu vinavyofanywa katika nyumba hizo pamoja na idadi kubwa ya wakaazi ambao hawajaripotiwa kwa sheha.

Naye Hassan Masuod Ali, Sheha wa Shehia ya Malindi, kwa niaba wa masheha wenzake alisema, watazidisha ushirikiano ili kuzitatua changamoto zilizopo ikiwamo usafi wa mazingira, wadaiwa sugu pamoja na wanaobadilisha nyumba kwa kufanyia biashara.

"Kwa kweli kwa nyumba za Kikwajuni za Mjerumani hali ngumu, mazingira machafu sana mwitu uliopo tunahofia kuwa kificho cha wahalifu na kuhofia maradhi ya mripuko," alisema.

Aliliomba shirika hilo kuweka mazingira rafiki katika nyumba za maendeleo ikiwamo ya Michenzani ili wahalifu wasizitumie kufanya uhalifu.



Wenye uziwi wakicheza ngoma ya Kibati wakati wakijiandaa kutumbuiza ukumbini katika sherehe za miaka 15 ya Jumuiya ya Wanawake wenye Ulemavu Zanzibar, hafla hiyo ilihudhuriwa na Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdullah jana. **PICHA: RAHMA SELEMANI**

# Wenye ulemavu kushirikishwa mipango ya maendeleo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, amesema Serikali ya Tanzania Bara na Visiwani Zanzibar inachukua hatua za kuwawezesha watu wenye ulemavu kukamilisha malengo yao na kutoa mchango wao katika kuliendesha taifa.

Akisoma hotuba ya Rais Samia Suluhu alipomwakilisha katika mkutano wa 15 wa Jumuiya ya Wanawake wenye Ulemavu Zanzibar uliofanyika visiwani humo jana, alisema serikali imetoa nafasi za uongozi kwa watu wenye ulemavu katika wizara mbalimbali na wanafanya kazi na kutimiza majukumu yao vizuri.

Alisema kuanzishwa kwa mabaraza ya watu wenye ulemavu katika wilaya yatasaidia upatikanaji na ujumuishaji wa masuala ya watu hao katika taasisi zote za umma na binafsi na kutetea haki na fursa zao.

"Pia Serikali ya Zanzibar imeanzisha mfuko wa maendeleo ya watu wenye ulemavu katika mwaka wa fedha 2023/2024 serikali imetenga bajeti Sh. milioni 200 na tayari fedha hizo zimeshaanza kuingizwa katika mfuko huo kwa lengo la kuwaendeleza kiuchumi," alisema.

Aidha, serikali pia imejenga shule mbili na bweni la wanafunzi Jendele, Unguja na Pujini, Pemba na shule hizo zina vifaa vya kisasa kuhakikisha wanapata fursa sawa za elimu kama watu wengine wasio na ulemavu.

Hemed alisema serikali itahakikisha wanawake wenye ulemavu wanashirikishwa kikamilifu katika mipango yake ya maendeleo ikiwamo katika sera na ushiriki wa siasa na uongozi hatua ambayo itawawezesha kujikomboa kiuchumi.

Alisema juhudi kubwa zimefanywa za kuwajengea uwezo wanawake na wasichana kwa ajili ya kufikia malengo na ndoto zao kiuchumi na kisiasa.

Aidha, alisema Serikali ya Zanzibar imetunga sheria ya watu wenye ulemavu namba nane ya mwaka 2022 ambayo itahakikisha haki na fursa zote zinapatikana kikamilifu na hakuna atakayechwa nyuma bila ya kujumuishwa. Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa UN, Zlatan Milisic, alisema wamefurahishwa na juhudi zinazochukuliwa na serikali zote mbili kuwawezesha watu wenye ulemavu kupiga hatua kubwa ya maendeleo na kuondokana na unyonge wa hali ngumu ya maisha.

"Umoja wa Mataifa unafurahishwa na juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuwainua wanawake wenye ulemavu kushiriki katika harakati za kisiasa na kiuchumi hatua ambayo ndiyo sehemu ya malengo endelevu ya dunia," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Jumuiya ya Wanawake Wenye Ulemavu (JUWAUZA), Bakari Hamad, alisema mafanikio makubwa yamepatikana katika kipindi cha miaka 15 tangu kuanzishwa kwa taasisi hiyo ikiwa ni kiungo kikubwa kwa wanawake wenye ulemavu kuyafikia malengo ya kiuchumi na maendeleo.

"Tunaadhimisha miaka 15 huku tukiwa na malengo yetu ya Jumuiya ya wanawake wenye ulemavu uwezekano wa maisha bora kiuchumi na maendeleo na kisiasa Zanzibar inawezekana," alisema.

Mpango wa mkakati wa miaka mitano ulizinduliwa ambao ni dira katika utekelezaji wa jumuiya hiyo ili kufikia malengo na unatarajiwa kugharimu jumla ya Sh. bilioni 14.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Hamza Hassan Juma alisema, serikali imeshafanya usajili kwa watu wenye ulemavu kwa ajili ya kuwatambua na kujua mahitaji yao. Alisema muswada wa sheria ya watu wenye ulemavu umeanza kufanya kazi zake ikiwamo kuwapo kwa baraza la watu wenye ulemavu na kuteuliwa kwa mtendaji wake ambaye miongoni mwa kazi zake ni uratibu kwa watu wenye ulamavu.

# Serikali yafungia zahanati tano kwa kukosa sifa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar, imezifungia zahanati tano kutotoa huduma za afya Zanzibar kwa sababu mbalimbali ikiwamo kutokuwa na wafanyakazi wenye uwezo na kuhatarisha afya za wananchi.

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake Mnazi Mmoja, Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema hatua hiyo inatokana na ziara iliyofanywa na wataalamu wa Wizara ya Afya na kubaini changamoto hizo.

Alisema wizara yake kupitia bodi ya hospitali binafsi ilifanya ukaguzi kwa vituo na hospitali binafsi katika wilaya zote kwa Unguja na Pemba ikiwa na lengo la kuangalia hali halisi ya uendeshwaji wa huduma hizo, mazingira ya hospitali, uwepo wa wafanyakazi pamoja na vifaa tiba.

Mazrui alisema upungufu uliobainika ni kutokuwa na wafanyakazi na kuajiri wafanyakazi wasiokuwa na sifa, hospitali hizo kuwapo katika mazingira machafu na kutoa huduma bila ya kufuata njia za kupunguza maambukizi kwa wagonjwa.

Alisema hospitali hizo zilizofungiwa kwa changamoto hizo ni pamoja na kituo cha Mawimbili, Mkwajuni Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa kukutwa hakina wafanyakazi wenye sifa kutoa huduma za afya.

Alivitaja vituo vingine ni Nyango iliyopo Kisauni, Neema kiliopo Tomondo na Glory Dispensary iliyopo Kinyasini.

Aidha, alisema kabla ya kufikia hatua hiyo wakaguzi walivipitia vituo vyote na hospitali binafsi kwa kubadilishana mawazo na kuona hali halisi katika utoaji wa huduma zao pamoja na kutoa maelekezo kwa utoaji huduma bora kwa wananchi.

"Ripoti iliyotolewa na bodi ya hospitali binafsi imeonesha kuwa jumla ya vituo na hospitali binafsi 113 vilikaguliwa, kati ya 155 sawa na asilimia 72.9 kwa kipindi cha Januari hadi Novemba, mwaka huu katika wilaya zote Unguja na Pemba," alisema.

Waziri Mazurui alisema kati ya hizo, hospitali tano na vituo vya afya vinne, zahanati 91 na 13 kliniki za huduma ya kwanza, na zahanati tano zilifungiwa kwa muda kutoa huduma kutokana na kubainika ukikuaji mkubwa wa uendeshaji hospitali binafsi ambao unahatarisha afya za wananchi wanaokwenda kutibiwa katika vituo hivyo.

Alisema kutokana na changamoto na kasoro mbalimbali zilizobainika, leo ataanza ziara ya kutembelea maduka ya kuuza dawa ili kuhakikisha dawa zinazouzwa ni salama kwa binadamu.

Alisema lengo ya serikali kuanzisha hospitali binafsi ni kuhakikisha wananchi wanapata tiba bora ili kujenga afya zao wanapopata matatizo ya kiafya.

# 'Kateni bima kwa ajili ya nyumba, biashara zenu'

NA Dennis Fussi

OFISA Masoko na Uhusiano wa Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC) ameshauri Watanzania kuwa na utamaduni wa kukatia bima mali zao zikiwamo nyumba na biashara ili kuepuka majanga ya moto yasiyotarajiwa.

Mohamed Shaaban alitoa rai hiyo juzi alipopokea tuzo ya huduma bora iliyotolewa na Jubilant Stewards of Africa jijini Dar es Salaam.

Shaaban alisema watu wengi wamekuwa na utamaduni wa kukatia bima vyombo vya moto yakiwamo magari, lakini wanasahau umuhimu wa kukatia bima nyumba na biashara zao zinazowaingizia vipato kuendesha maisha yao.

"Kwa maisha ya sasa, bima zote zina umuhimu, zikiwamo za nyumba, bima dhidi ya wizi, bima ya kusafirisha mizigo na nyinginezo.

"Tumeshuhudia wafanyabiashara wakipoteza mitaji yao pale inapotokea majanga ya moto au wizi kutokana na kutokata bima," alionya.

Alisema tuzo hiyo imedhihirisha ubora wa huduma zinazotolewa na shirika hilo kwa upande wa Zanzibar na Tanzania Bara, wakiwafikia watu wengi katika upatikanaji huduma hiyo.

"Tuzo hii inatupa faraja sana na inaonesha ni kwa namna gani watu wanatumia huduma za bima kwa ajili ya maendeleo yao na taifa kwa ujumla," alisema.

Tuzo hizo zilishirikisha kampuni mbalimbali ndani na nje ya nchi, ambazo zilipewa tuzo katika kutambua mchango wao wa kutoa huduma kwa wananchi.

Akizungumza katika tuzo hizo, mgeni rasmi, Dk. John Shusho ambaye ni Balozi wa Amani, alisifu jitihada za kampuni mbalimbali katika kuleta mabadiliko ya uchumi kupitia ushindani wa kibiashara na utoaji huduma bora.

Alitaka kampuni kutumia ubunifu unaotokana na ukuaji wa teknolojia ili kuendelea kuwa na ushindani katika soko la dunia.

"Wakati tunafurahia maendeleo tuliyonayo, ni lazima tutambue kuwa uongozi bora hupelekea ukuaji wa uchumi kupitia uwajibikaji, uwazi na utoaji uamuzi sahihi," alisema.

Pia alitaka kampuni hizo kurudisha sehemu ya faida yao kwa jamii, akisema kuwa ukuaji wa biashara haupimwi kupitia faida kubwa pekee, bali kupitia michango mbalimbali inayotolewa na kampuni hizo katika kuleta mabadiliko ya jamii.



Mkurugenzi wa TARI Mlingano Muheza, Tanga, Dk. Catherine Senkoro (kushoto), akielezea utendaji kazi wa TARI mwishoni mwa wiki baada ya kukagua jengo la maabara mpya ya utafiti wa mbegu na udongo. Wa pili kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo, Katibu Tawala Muheza (wa tatu kushoto), Mohamed Mfaki na Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Muheza, Jumaa Mhina (kulia). **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Ataka jamii iwe na hofu ya Mungu

Na Denis Mambya, MOROGORO

KUTOKUWA na hofu miongoni mwa wanajamii imetajwa kuwa moja ya sababu inayochagiza matukio ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia kutokana na matukio hayo kuzidi kuibuka kila kukicha nchini.

Hassan Awf, Ofisa Ustawi wa Jamii kutoka kituo cha Amani Center For Street Children, chenye makao yake jijini Arusha, kinachohusika na kuwasaidia watoto waishio katika mazingira magumu nchini wakati akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu, mwishoni mwa wiki.

Hassan alisema mara kadhaa huzishirikisha mamlaka husika kama Ustawi wa Jamii na Jeshi la Polisi kupitia dawati la jinsia na watoto ili kuibua na kuhakikisha ya kwamba watu wa aina hiyo katika jamii wanachukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kufikishwa mahakamani.

George Fabian, mkazi wa Kata ya Kihonda, Manispaa ya Morogoro, alibainisha kwamba katika jamii kumekuwa na matukio ya kikatili hasa kwa watoto wadogo na yatima wasio na uwezo wa kujieleza na kilio kwa watoto hao dhidi ya ukatili umekuwa ukifanywa na watu wasio na hofu ya Mungu.

Amina Hassan, mkazi wa Mtaa wa Kata ya Mji Mpya, Manispaa ya Morogoro, alisema ukatili na unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya wanawake na makundi maalum, hutokea mara kwa mara katika jamii na hutekelezwa na watu walio na uwezo wa kifedha na madaraka.

Swalahe Hamza, mkazi wa Kata ya Bigwa, alisema katika jamii hii watumishi wa Mungu wakiwamo mashehe na wachungaji wanatakiwa kuwaonya na kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia wawapo katika ibada ili jamii imrudie Mwenyezi Mungu.

Asha Hamidu mkazi wa Kata ya Kilakala, aliutaja ujinga na ukosefu wa elimu ya kutosha juu ya vitendo vya ukatili wa kijinsia unachangia kwa kiasi wanajamii kutokuzitambua athari zitakanazo na ukatili wa kijinsia na kuwaomba wanajamii wenzake kutafakari kwa kina maumivu yanayowapata waathirika wa vitendo hivyo.

Jamii inatakiwa kukumbuka kizazi hiki kinatakiwa kurithishwa mema na mazuri ili kuwa na hofu mbele ya Mungu na kuijenga Tanzania yenye kizazi bora na chenye kumtii na kumpendeza mwenyezi Mungu wakati wote.

## Prof. Mganilwa ajivunia miaka 12 mafanikio NIT

Na Mwandishi Wetu, MOSHI

BAADA ya kukitumikia kwa miaka 12 akiwa Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Prof. Zacharia Mganilwa sasa anastaafu nafasi hiyo ya uongozi, akijivunia mafanikio ikiwamo ongezeko kubwa la wanafunzi, ushirikiano na maboresho katika utendaji kazi.

Amesema kuwa chini ya uongozi wake, NIT sasa ni mojawapo ya taasisi za elimu ya juu nchini na katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati ambazo zinatoa viwango bora katika elimu kwenye sekta ya usafiri na usafirishaji, kikivutia waajiri.

Katika mazungumzo na waandishi wa habari mwishoni ma wiki, Prof. Mganilwa ambaye bado ni mtumishi wa umma hadi 2028 atakapofikia umri wa miaka 65 wa kustaafu kwa lazima, alisema adhima yake baada ya kustaafu nafasi hiyo ya ukuu wa chuo angependa kuendelea kusalia NIT ili kutoa elimu na ujuzi kwa vijana na kukifanya kuwa na uwezo wa kutoa Shahada za Uzamivu (Ph.D) kabla ya kustaafu rasmi miaka mitano ijayo.

Alisema kuwa alipojiunga na NIT mwaka 2011/12 kama mkuu wa chuo, idadi ya programu ambazo zilikuwa zinatolewa na chuo kwa upande wa shahada zilikuwa mbili tu, lakini sasa kuna kozi 16, programu za stashahada (diploma) zilikuwa mbili tu mwaka 2011/12, lakini sasa kozi hizo 25.

Kuhusu wanafunzi, alisema kuwa alipoanza kazi mwaka 2011/12, idadi ya wanafunzi ilikuwa 575, sasa wana wanafunzi 16,000.

"Katika muda wangu wote wa miaka 12, taasisi ina jumla ya wafanyakazi 400 kulinganishwa na miaka 12 iliyopita wakati idadi ya wafanyakazi ilikuwa 113.

"Mwaka 2011 nilipofika hapa, taasisi ilikuwa na wataalamu wa usafiri wanane tu, lakini sasa wataalamu hao ni zaidi ya 150," alifafanua.

Kuhusu mapato ya ndani, alisema NIT imeongeza mapato yake kutoka Sh. milioni 800 mwaka wa fedha 2011/12 hadi Sh. bilioni 25 mwaka 2021/22 na bajeti ya taasisi iliimarika kutoka Sh. bilioni tano hadi Sh. bilioni 96 kwa mwaka huu wa fedha.

"Nilipoanza kazi mwaka 2011, taasisi ilikuwa inatoa mafunzo katika mode moja tu wa usafiri (barabara), lakini sasa aina zote tano zinatolewa hapa NIT, kwa maana ya barabara, reli, anga, maji na bomba la mafuta.

"Chini ya uongozi wangu, taasisi iliweza kupata ndege mbili aina ya Cessna Skyhawk zenye injini moja zenye thamani ya dola za Marekani milioni 1.057 kutoka Kampuni ya Textron Aviation Inc. yenye makao yake Marekani kwa ajili ya kozi za usafiri wa anga ikiwamo urubani.

Pia anajivunia kuanzisha Kituo cha Umahiri katika Uendeshaji wa Usafiri wa Anga na Usafiri (CEATO) kilichopata msaada kutoka Benki ya Dunia chini ya usimamizi wa Mradi wa Ujuzi wa Mageuzi na Utangamano wa Kikanda wa Afrika Mashariki (EASTRIP) wenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 49.

HABARI KIMATAIFA

## Putin sasa ni mgombea huru

**Kremlin,** RUSSIA

VLADIMIR Putin atagombea tena katika uchaguzi wa urais kama mgombea huru, shirika la habari la RIA linaloungwa mkono na serikali limesema, mwishoni mwa wiki.

Shirika hilo pia, liliwanukuu wabunge wawili wakuu wanaomuunga mkono Kremlin.

Kwa zaidi ya miongo miwili, Vladimir Putin ametangaza kuwa atawania muhula mwingine wa miaka sita Machi mwaka ujao, katika uchaguzi anaotarajiwa kuushinda.

Hatagombea kama mgombea wa chama tawala cha United Russia (UR), ingawa anaungwa mkono kikamilifu, lakini kama mgombea huru, Andrei Turchak, Ofisa Mkuu wa chama hicho, alinukuliwa na shirika la habari la RIA.

Sergei Mironov, Ofisa wa Chama cha Just Russia, anayemuunga mkono Vladimir Putin, pia ameliambia shirika la habari la RIA kwamba, rais atagombea kama mtu huru na kwamba saini zitakusanywa kwa niaba yake.

Vladimir Putin, mwenye umri wa miaka 71, anasema uchaguzi huu ni wa kawaida.

Akiungwa mkono na serikali, vyombo vya habari vya umma na kutokuwapo kwa upinzani kwa maoni ya umma, ushindi wake unazingatiwa.

Wafuasi wake wanasema kuwa alirejesha utulivu, sifa ya kitaifa na baadhi ya ushawishi ambao Russia ilipoteza baada ya kuanguka kwa Umoja wa Kisovieti.

Pia wanahalalisha vita yake nchini Ukraine, ambayo anaiita operesheni maalum ya kijeshi.

Ukandamizaji wa miaka mingi wa wapinzani na wakosoaji, ulioimarishwa na sheria mpya zinazoenea, umesababisha vifungo virefu au kulazimishwa kutoroka nje ya nchi kwa wapinzani.

Nafasi za wapinzani zimepungua polepole. Siku ya Ijumaa Vladimir Putin alitoa onyo dhidi ya uingiliaji wowote wa kigeni katika kampeni ya urais iliyopangwa Machi 2024 kwa muktadha uliongaziwa na mzozo wa Ukraine na ukandamizaji wa wapinzani wote.

Wakati wa mkutano wa televisheni na viongozi wa chama waliopo Duma, ikulu ndogo ya Bunge, alisema: "Uingiliaji wowote wa mambo ya ndani ya Urusi utaadhibiwa vikali kwa mujibu wa sheria za Russia.

"Tunatetea uhuru wa raia wetu, mamlaka yao na haki yao ya kuchagua mustakabali wao.

Raia wa Russia ndio chanzo pekee cha nguvu katika nchi yetu."

Putin alitoa shukrani zake kwa wajumbe wa vyama vya bunge wanaounga mkono operesheni maalum ya kijeshi nchini Ukraine, akisisitiza kujitolea kwao kwa Russia na msaada wao kwa wanajeshi na familia zao. **RFI**

UCHAGUZI MKUU KESHO KUTWA

# DRC, amani yatilia shaka ushiriki upigaji kura eneo la Mashariki

**KINSHASA,** DRC

**Imesalia siku moja, kabla uchaguzi mkuu wa Desemba 20, mwaka huu (keshokutwa).**

ZAIDI ya wapigakura milioni 40 wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), wanajiandaa kujitokeza keshokutwa na kuchagua viongozi wao kuanzia ngazi ya urais, ubunge na madiwani.

Shauku kubwa iliyopo miongoni mwa wananchi ni uchaguzi huo kufanyika kwa amani.

Kuelekea uchaguzi huo, pamoja na shughuli za kutafuta kipato kuendelea mjini Kinshasa na katika maeneo mengine ya nchi, wasiwasi upo kwa waliopo Mashariki mwa DRC, iwapo watashiriki haki hiyo.

Imesalia siku moja, kabla uchaguzi mkuu wa Desemba 20, mwaka huu (keshokutwa).

DRC ni miongoni mwa nchi tajiri barani Afrika kutokana na rasilimali zilizopo nchini humo.

Hata hivyo, nchi hiyo kwa miongo kadhaa imekuwa ikikabiliwa na tatizo la usalama hasa mashariki mwa nchi.

Tume Huru ya Uchaguzi (CENI), imesema, licha ya changamoto zilizopo hasa katika ushambazaji wa vifaa vya kupigia kura katika baadhi ya maeneo, lakini tarehe ya uchaguzi haitabadilika. **TRT**



Baadhi ya vijana wakiwa katika kampeni mjini Kinshasa nchini DRC. Zaidi ya wapigakura milioni 40 wanatakiwa kujitokeza kuchagua viongozi wao kuanzia ngazi ya urais, ubunge na udiwani. Kampeni zimepamba moto, huku ikisalia siku moja tu kabla ya uchaguzi huo kufanyika. **PICHA: TRT**

# 'Huenda ugonjwa wa TB ukatoweka duniani'

**Pretoria,** AFRIKA KUSINI

UTAFITI wa hivi karibuni kuhusu matibabu mapya ya kifua kikuu (TB) yanayokinzana na dawa, BPaL, unaonyesha kuwa ina kiwango cha tiba zaidi ya asilimia 90, ikiwa na vidonge vichache na muda mfupi wa matibabu wa miezi sita.

Wagonjwa sasa wanaweza kumeza vidonge viwili kwa siku kadhaa za wiki kwa kutumia dawa mpya ya TB.

Kwa miezi kadhaa, Happy Ntsibande aliogopa dawa ile ile ambayo maisha yake yalitegemea.

Baba huyo wa watoto watatu mwenye umri wa miaka 50, alikuwa akipambana na TB, ambayo matibabu yake yangeweza kudumu kwa takriban miaka miwili.

Nilikuwa nikinywa hadi vidonge 24 kila siku, ikiwa ni pamoja na kinywaji cha unga kwenye sacheti iitwayo Palser - sharubati ambayo ina ladha mbaya, haiwezi kupungua bila mtindi.

Happy anaiambia TRT Afrika.

Alihamishiwa katika Hospitali ya Sizwe inayomilikiwa na serikali huko Johannesburg wakati daktari wake katika Hospitali ya Kusini, alikufa kutokana na aina mbaya zaidi ya TB inayojulikana kama kifua kikuu kinachokinza dawa (XDR-TB).

Mzigo mkubwa wa TB duniani umewafanya wanasayansi kutafuta dawa bora zaidi, zisizo na sumu na fupi ili kuhakikisha watu wengi zaidi wanapata matibabu.

Kulingana na ripoti ya hivi punde ya kifua kikuu duniani, TB iliua watu milioni 1.3 mwaka 2022 na kuwa muuaji wa pili baada ya Uviko-19 (juu ya VVU/UKIMWI). Inaonyesha kuwa zaidi ya watu milioni 10 wanaugua TB kila mwaka.

TB ni ugonjwa unaoenezwa kwa njia ya hewa kwa kukohoa au kupiga chafya. Ni ugonjwa mgumu kuponya, unaohitaji wagonjwa kuchukua mchanganyiko wa dawa kwa angalau miezi minne hadi sita.

Wagonjwa wanaweza kushindwa kudhibiti ugonjwa wa TB kutokana na ugonjwa wenyewe kuwa sugu iwapo wataruka dozi au kushindwa kukamilisha matibabu kamili.

Aina zinazokinza dawa zinaambukiza vile vile. Kifua kikuu sugu kinapoingia katika kaya, kila mtu yuko hatarini, alisema Dk. Moronfolu Olugbosi, Mkurugenzi Mkuu wa Maendeleo ya Kliniki katika TB Alliance.

"Kukomesha TB ifikapo 2033 au tarehe yoyote ni suala la utashi wa kisiasa. Linaweza kufanyika lakini kwa uwekezaji wa kutosha wa kimataifa," alisema Dk. Olugbosi.

Duniani, inakadiriwa watu 410,000 walipata TB sugu kwa dawa nyingi (MDR-TB) mnamo 2022 lakini ni wagonjwa wawili tu kati ya watano waliotibiwa.

Majaribio yalifanyika Indonesia, Kyrgyzstan, Ufilipino, Uzbekistan na Vietnam, nchi zilizo na mzigo mkubwa wa maambukizi ya TB sugu kwa dawa.

Matokeo yaliyowasilishwa kwenye Mkutano wa Muungano wa Afya ya Mapafu huko Paris, Novemba, mwaka huu, yalionyesha kwamba dawa ilikuwa na kiwango cha tiba cha asilimia 95 kwa wagonjwa 319 ambao walikuwa wamemaliza matibabu na ufuatiliaji baada ya matibabu. **TRT**

# AFISA MICHEZO MARA MGENI RASMI FAINALI UMOJA CUP 2023

Na Mwandishi Wetu, RORYA

BAADA ya timu nne zilizotinga hatua ya nusu fainali ya michuano ya Umoja Cup 2023 wilayani Rorya kufahamika, hatimaye waandaaji wa mashindano hayo wametangaza rasmi fainali itapigwa mwishoni mwa mwezi huu, huku mgeni rasmi akitarajiwa kuwa Afisa Michezo wa Mkoa wa Mara, Makondo Makondo.

Katika michezo ya pili ya robo fainali ya michuano hiyo inayodhaminiwa na mdau mkubwa wa michezo wilayani Rorya, Peter Owino, ambayo ilipigwa mwishoni mwa wiki kwenye Uwanja wa Maji Shirati Sota, Wanamaji FC waliwalowesha Mafundi FC kwa bao 1-0, huku Bubombi FC wakiwatupa nje ya mashindano Gonga FC kwa mikwaju ya penalti.

**Wanamaji FC ambao ndio wenyeji wa mashindano ya Umoja Cup 2023, walifanikiwa kutinga nusu fainali mbele ya mashabiki wao, shukrani zikimwendea nahodha wao, Tumaini Atola, kwa kufunga bao hilo pekee kwa mkwaju wa penalti katika dakika ya saba ya mchezo.**

Mwamuzi wa mchezo huo, Omary Galus, aliamuru mkwaju huo wa penalti baada ya beki wa Mafundi FC, Ooko Wnga, kumchezea vibaya, Nasibu Peter wa Wanamaji FC ndani ya eneo la hatari.

Hata hivyo, mfungaji wa penalti hiyo ya Wanamaji, Atola, alipewa kadi nyekundu katika dakika ya 73 ya mchezo baada ya kukabana koromeo na mchezaji wa Mafundi FC, Erenest Otieno, ambaye naye alikutana na adhabu hiyo kutoka kwa refa Galus.

Kwa kadi hiyo nyekundu Atola sasa ataukosa mchezo wa nusu fainali dhidi ya Bubombi FC na ule wa fainali endapo timu yake itafanikiwa kuwatoa Wanamaji FC.

Katika mchezo mwingine wa robo fainali ya mwisho kati ya vijana wa Mpakani, Bubombi FC na wale wa Nyahongo, Gonga FC, ilimalizika kwa mshindi kupatikana kwa njia ya mikwaju ya penalti, baada ya dakika 90 kukamilika miamba hiyo ikitoshana nguvu kwa kufungana mabao 3-3. Katika hatua ya mikwaju ya penalti Bubombi walibuka kidedea kwa 3-2.

Mwenyekiti wa Mashindano hayo, Ochieng Meli, akizungumza na mwandishi wetu mwishoni mwa wiki, alisema timu mbili kutoka Kata ya Mkoma Wilaya ya Rorya, Kabwana FC na Shirati Mji FC, ambazo awali zilitangulia nusu fainali, ndizo zitakazofungua mechi za hatua hiyo katika Uwanja wa Maji Shirati Sota, Alhamisi wiki hii huku Ijumaa nusu fainali ya pili ikipigwa uwanjani hapo pia kati ya Wanamaji dhidi ya Bubombi FC.

Aidha, Ochieng alisema fainali ya michuano hiyo itafanyika mwisho wa mwezi huu, Desemba 31 katika uwanja huo huku mgeni rasmi akitarajiwa kuwa Afisa Michezo wa Mkoa wa Mara, Makondo.



Kikosi cha Wanamaji FC, kinachotarajiwa kuvaana na Bubombi FC katika mchezo wa nusu fainali ya michuano ya Umoja Cup Rorya 2023, utakaopigwa Uwanja wa Maji Shirati Sota, Ijumaa wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



## *Jesca apania kumchakaza Sarah*

Na Shufaa Lyimo

BONDIA wa Ngumi za Kulipwa nchini, Jesca Mfinanga (pichani), amesema yupo imara na tayari kupanda ulingoni kuzichapa dhidi ya Sarah Alex katika pambano la usiku wa Mabingwa linalotarajiwa kufanyika Desemba 26, mwaka huu katika Ukumbi wa Ubungo Plaza, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, akiwa anaendelea kufanya mazoezi yake ya mwisho mwisho, Jesca alisema anamfahamu vema mpinzani wake huyo hivyo amejiandaa vizuri kwa ajili ya pambano hilo.

"Nipo vizuri kukutana na mpinzani wangu siku hiyo, ninaendelea kufanya mazoezi ambayo ninaamini nitawapa burudani nzuri mashabiki wangu," alisema Mfinanga.

Aliongeza kwa kuwataka mashabiki wake kukaa mkao wa kula raha siku hiyo kwani hana wasiwasi kukutana na Sarah kutokana na uzoefu alikuwa nao.

Aidha, aliwataka mashabiki wake kujitokeze kwa wingi kushuhudia pambano hilo ambalo linatarajiwa kuwa na upinzani mkubwa.

Katika hatua nyingine, aliwataka wanawake wajitokeze kwa wingi kujifunza mchezo wa ngumi kwani ni wa kawaida kama ilivyo michezo mingine.

"Ninashauri wanawake wenzangu wajifunze ngumi, wanatakiwa wafahamu ni mchezo wa kawaida kama ilivyo michezo mingine, vile vile unawasaidia kupata ajira," alisema bondia huyo.

## Biashara United kurudi tena Ligi Kuu

Na Adam Fungamwango

TIMU ya Biashara United imeonekana kupania kutaka kurejea Ligi Kuu baada ya kuishindilia Pan African mabao 4-0, na kupanda hadi nafasi ya pili ya Ligi ya Championship inayoendelea nchini.

Katika mechi hiyo iliyochezwa juzi Uwanja wa Karume, Musoma, mkoani Mara, Biashara United imefikisha pointi 30, ikiwa imemaliza mechi zake 15 za mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo inayoongozwa na KenGold yenye pointi 32.

Straika raia wa Uganda, Boban Zirintusa, alifunga mabao matatu 'hat-trick' katika mechi hiyo dakika ya 15, 25 na 50, huku Paschal Masinde akiutumbukiza mwenyewe mpira alipokuwa akijaribu kuokoa hatari kutoka kwa Benson Masinge.

Biashara United ilipanda Ligi Kuu kwa mara ya kwanza mwaka 2018, lakini iliteremka 2022, huku ikiwa imeshaweka rekodi ya kucheza mechi za kimataifa, ikifanya hiyo 2021 ilipocheza mechi dhidi ya Al Ahli Tripoli ya Libya nchini na kushinda mabao 2-0, Oktoba 15 jijini Dar es Salaam, lakini ikashindwa kwenda ugenini na kutolewa kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Matokeo ya mechi zingine za Ligi ya Championship, Green Warriors ilichapwa bao 1-0 dhidi ya Mbeya Kwanza, Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, Pamba ikatoka suluhu dhidi ya TMA Uwanja wa Nyamagana, Mwanza, Mbeya City iliifunga Polisi Tanzania bao 1-0, Uwanja wa Sokoine, Mbeya na Transit Camp ikiwa Uwanja wa Jamhuri, Morogoro, iliiadhibu Ruvu Shooting mabao 2-0.



## ZISIKUPITE

### SALAH ALENGWA SAUDIA

Ligi Kuu ya Saudi Arabia (Saudi Pro League), itafanya majaribio mapya kumsajili mshambuliaji wa Liverpool na Misri, Mohamed Salah msimu ujao huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, akiwa mlengwa mkuu wa ligi hiyo. ***(Mail)***

### CARVALHO KUREJEA FULHAM

WINGA wa Ureno, Fabio Carvalho, yuko tayari kurejea Fulham ikiwa Liverpool wanaweza kumwita mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 kutoka kwa mkopo katika klabu ya RB Leipzig. ***(Mirror)***

### IVAN AITAKA ARSENAL

MSHAMBULIAJI wa Brentford na England, Ivan Toney mwenye umri wa miaka 27, anasemekana kufurahishwa na uwezekano wa kujiunga na Arsenal. ***(Fabrizio Romano via Mail)***

### BELLINGHAM AFUATILIWA

MASKAUTI kutoka klabu za Ligi Kuu England ikiwa ni pamoja na Liverpool, Arsenal na Chelsea, zimeripotiwa kumfuatilia winga wa England, Jobe Bellingham mwenye umri wa miaka 18 anayeichezea Sunderland. ***(Ekrem Konur)***

### ECHEVERRI AWINDWA CITY

CHELSEA na Manchester City zimejiunga na Barcelona katika kinyang'anyiro cha kumsajili kiungo wa kati wa Argentina, Claudio Echeverri mwenye umri wa miaka 17 kutoka River Plate. ***(Mirror)***

### MILAN WAMTAKA LENGLET

AC Milan imewauliza Barcelona taarifa kuhusu mlinzi wa kati wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 28, Clement Lenglet, ambaye yupo kule Aston Villa. ***(Caughtoffside)***

### DE BEEK NA FRANKFURT

KLABU ya Eintracht Frankfurt itakuwa na chaguo la kumnunua kiungo wa kati wa Uholanzi, Donny van de Beek mwenye umri wa miaka 26, kutoka Manchester United kwa chini ya euro milioni 10 msimu wa majira ya joto, akishatua hapo kwa mkopo Januari. ***(Sky Germany kupitia Florian Plettenberg)***

### DAU LA PHILLIPS HILI HAPA

KLABU ya Manchester City ilitaka Everton kulipa ada ya mkopo ya pauni milioni 7.5 kwa kiungo wa kati wa England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 28, wakati wa dirisha la usajili la majira ya joto. ***(Football Insider)***

### PEAZ RASMI CHELSEA

KIUNGO wa Ecuador mwenye umri wa miaka 16, Kendry Paez atafanya mazoezi na Chelsea wiki ijayo. 'The Blues' walimsajili kutoka Independiente del Valle msimu uliyopita kwa makubaliano ya kujiunga na klabu hiyo atakapotimiza umri wa miaka 18. ***(Telegraph)***

### VERMEEREN LULU ARSENAL

KLABU za Arsenal na Tottenham Hotspur zimetuma maskauti wao kumfuatilia kiungo wa Ubelgiji Arthur Vermeeren mwenye umri wa miaka 18. ***(90 min)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# WASAUDIA HAWAJAKATA TAMAA KUMSAJILI MBAPPE

**RIYADH,** Saudi Arabia

MKURUGENZI wa Ligi Kuu ya Saudi Arabia, Saudi Pro League, amethibitisha kwamba, maofisa wa klabu moja ya huko bado wapo katika "mazungumzo ya wazi" na Kylian Mbappe anapokaribia mwisho mwa mkataba wake na Paris Saint-Germain.

**Kutokana na kuthibitisha kwamba hataongeza nyongeza katika mkataba wake wa sasa baada ya msimu wa majira ya joto wa 2024, Mbappe aliwekewa dau na Klabu ya Al Hilal la euro milioni 300 ambalo lilikubaliwa na PSG.**

Hata hivyo, Mbappe aliweka wazi kuwa hakuwa na nia ya kuhamia Mashariki ya Kati wakati huo na mazungumzo yalikatika ghafla.

Tangu wakati huo, Mbappe amerejea kwenye kikosi cha PSG baada ya kukubali bonasi ya euro milioni 80 ambayo alipaswa kubakia tu katika klabu hiyo msimu huu.

Alisisitiza hadharani kuwa ana mpango wa kubakia PSG kwa kipindi kizima cha msimu huu, lakini nyuma ya pazia inaeleweka aliweka wazi kuwa hana mpango wa kuongeza mkataba zaidi.

Real Madrid ambayo kwa muda mrefu imekuwa ikimwania, inatumaini kumpata Mbappe kwa uhamisho wa bila malipo mkataba wake utakapomalizika, lakini Mfaransa huyo anaweza kuzungumza na klabu yoyote mapema Januari Mosi, 2024 na Mkurugenzi wa SPL, Michael Emenalo, amedokeza uwezekano wa usajili wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24.

"Ni mazungumzo ya wazi, lakini hatujui anataka kufanya nini," alisema Emenalo akiiambia Sky Sports News.

"Msimamo wetu uko wazi sana. Ikiwa kuna nia ya kuwa sehemu ya kile tunachojaribu kujenga sasa au kwa siku zijazo, huwezi kukataa fursa ya kuona kama Mbappe anaweza kujiunga nasi. Kylian ni mtu ninayempenda kama mchezaji."

Alipoulizwa ni kwa ukaribu kiasi gani Al Hilal, ambayo ilimsajili Neymar na baadaye majira ya joto itamsajili Mbappe, Emenalo alisema: "Lolote linawezekana.

"Siwezi kusema mazungumzo yalikuwa ya kina kiasi gani, lakini kulikuwa na maoni ya kwamba kama alikuwa tayari kuja, kulikuwa na klabu tayari kutoa nafasi kwa ajili yake."

●●● Lolote linawezekana. Siwezi kusema mazungumzo yalikuwa ya kina kiasi...

# GUARDIOLA AGEUKA MBOGO



**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola aliibwatukia timu yake baada ya ulinzi wao wa kizembe na kusababisha penalti ya dakika za mwisho iliyogharimu ushindi uliohitajika sana na kusababisha sare ya 2-2 dhidi ya Crystal Palace Jumamosi, akisema walistahili matokeo hayo.

"Si bahati mbaya, tulistahili," alisema Guardiola mwenye hasira akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Tunatoa pointi mbili. Unapotoa penalti hii, unastahili kufungwa. Unaona nafasi tulizotengeneza na kufungwa, ni sawa na msimu huu wote, lakini hatuna uwezo wa kufunga mechi. Hiyo ndiyo shida."

City wameonekana kutokuwa kwenye kiwango chao baada ya michezo sita wakiwa na ushindi mmoja pekee.

Jack Grealish na Rico Lewis walifunga kipindi cha kwanza kwenye Uwanja wa Etihad Jumamosi, lakini Jean-Philippe Mateta akachomoa kwa Palace na kisha Michael Olise kufunga penalti dakika ya 95 baada ya Phil Foden kumchezea vibaya Mateta kwenye eneo la hatari.

Sare hiyo iliwaacha Man City wakiwa nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu wakiwa na pointi 34, lakini wamecheza mchezo mmoja zaidi ya timu tatu zilizo juu yao: Liverpool, walio kileleni kwa pointi 37, Arsenal na Aston Villa, ambazo zote zilicheza jana Jumapili.

"Mwisho ni lazima uwe na subira," Guardiola alisema kuhusu matokeo hayo ya kukatisha tamaa.

"Lakini kwa kweli katika hatua ya kwanza (Palace) wanakimbia na kufunga bao na dakika ya mwisho tunawapa penalti. Katika eneo la 18 lazima uwe mwangalifu na hatukuwa. Hatufanyi hivyo, wanastahili kushinda."

# Pochettino sasa roho kwatu

**LONDON,** England

MAURICIO Pochettino alisifu mwitikio wa Chelsea baada ya vipigo viwili mfululizo vya Ligi Kuu England walipopata ahueni na kuifunga Sheffield United mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Stamford Bridge, Jumamosi.

Wenyeji walipambana kutokana na mchezo mgumu wa kipindi cha kwanza wakiwa wanatoka kufungwa na Manchester United na Everton kwa kupachika mabao mawili ya haraka katika kipindi cha pili kupitia kwa Nicolas Jackson na Cole Palmer.

La kwanza lilipatikana kutokana na kazi nzuri kati ya Palmer na Raheem Sterling, mchezaji aliyesajiliwa majira ya joto kutoka Manchester City. Na Palmer ndiye alikuwa mbunifu dakika chache baadaye kwa bao la Jackson.

Baada ya mchezo huo Pochettino alisema: "Nadhani tulizungumza mengi wiki moja baada ya Everton kuhusu kuhitaji mabadiliko makubwa.

"Ilikuwa muhimu kuthibitisha kwamba tuko katika hali nzuri. Timu katika kipindi cha kwanza ilichanganyikiwa kwa sababu hatukuweza kupata njia ya kupita kizuizi cha Sheffield United.

"Hatukuonesha uwezo wa kubadilika na ilikuwa rahisi kwao kutambua nafasi yetu na kutuzuia na kutufanya tuweke mpira katika nafasi ambazo zilikuwa rahisi kwao kuzizima.

"Kipindi cha pili tulikuwa bora zaidi, tulirekebisha mambo. Timu ilianza kupata nafasi nzuri ya kucheza, kuunganisha vizuri zaidi.

"Cole kutoka kulia, akiingia kwenye nafasi, alianza kuunganishwa vema na wachezaji wenzake na kuwa mchezaji ambaye tunataka kumtumia."






# Xavi afadhaika kwa sare

**VALENCIA,** Hispania

XAVI Hernandez aliyekasirika alilaumu kukosa nafasi huku mbio za kutoshinda za Barcelona zikiongezwa hadi mechi tatu kwa sare ya 1-1 dhidi ya Valencia kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Jumamosi.

Joao Felix alianza kuifungia Barca kwenye Uwanja wa Mestalla, ambao walilazimishwa kulipa uzembe wao wakati Hugo Guillamon alipoisawazishia Valencia dakika ya 70.

Barca walipata nafasi zaidi za kushinda mchezo huo mwishoni, huku Ferran Torres na Raphinha wote wakipoteza nafasi za wazi za kufunga.

"Nimefadhaika sana na nina huzuni kwa sababu tulitengeneza nafasi nyingi," alisema Xavi baada ya mchezo kumalizika.

"Tulikosa nafasi nyingi. Nadhani ndicho kilichotokea msimu mzima.

"Tunatawala michezo. Tumecheza vizuri sana leo (juzi). Inasikitisha kwa sababu hatufanyi vizuri. Nadhani tumepata nafasi tano, sita au saba na hatukufunga.

"Ni kile ambacho kimetokea msimu mzima. Tunahitaji kuendelea, ni pointi moja tu, ambayo haitoshi kwetu. Inasikitisha kwa sababu tulicheza vizuri kushinda mchezo huu."

Barca sasa wako nyuma ya viongozi Girona kwa pointi sita, ambao wanaweza kusonga mbele kama wataifunga Alaves leo, Jumatatu.

Real Madrid nao watasonga mbele kwa pointi saba mbele ya Barca ikiwa jana Jumapili waliifunga Villarreal.

Hata hivyo, baada ya kufungwa mfululizo dhidi ya Girona na Antwerp, Xavi alisisitiza kwamba aliona inatosha na katika mchezo dhidi ya Valencia ungekuwa chanya.

"Tunahitaji kuendelea, ni msimu mrefu," aliongeza.

"Sasa tuone nini kitatokea katika michezo ijayo, lakini tunahitaji kuimarika, bila shaka, si kutengeneza nafasi na kufunga."

# SHEKHAN AMTAJA BACCA, MUDATHIR KUTUA YANGA

Na Adam Fungamwango

MCHEZAJI mpya wa Yanga, Shekhan Ibrahim Khamis, aliyetambulishwa rasmi Ijumaa iliyopita na Jumamosi kujitokeza Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam kusalimia mashabiki wa timu hiyo, amesema ameamua kujiunga na timu hiyo kutokana na kuvutiwa na Mudathir Yahaya na Ibrahim Hamad 'Bacca.'

Akizungumza kwa mara ya kwanza baada ya kujiunga na klabu hiyo akitokea JKU ya Zanzibar, alisema kulikuwa na ofa nyingi za ndani na nje ya nchi baada ya kuonekana kwenye michuano ya CECAFA kwa vijana, lakini ameamua kuwafuata kaka zake wanaotoka Zanzibar kwenye kikosi cha Yanga kwa ajili ya kumpa moyo, na miongozo.

"Ni kweli timu nyingi zilinitaka, siyo hapa tu hata nje ya nchi, lakini nilipopigiwa simu na Makamu rais wa Yanga, Arafat Haji, sikujiuliza tena mara mbilimbili kwa sababu nikajua huko nikienda nitakuwa salama zaidi. Kuna kaka zangu, Mudathir na Bacca, yaani kama niko nyumbani, kwanza napenda sana uchezaji wao, halafu pia nilikuwa na hamu sana kucheza nao timu moja, nikajua kabisa nitapata washauri wazuri," alisema mchezaji huyo.

**Alisema amejiunga na Yanga akiwa hana wasiwasi wa kupoteza kipaji chake kwa sababu ana uhakika atafanya mazoezi kwa bidii kwa ajili ya kumshawishi kocha na pia anajiamini.**

"Mimi natumia sana mguu wa kushoto, na nacheza winga namba saba, nane na 10, nilianza kucheza soka kwenye akadem ya JKU kwa miaka sita, nimeshawahi pia kucheza michuano ya Copa Cocacola Mtwara," alisema mchezaji huyo.

Shekhan anakuwa mchezaji wa kwanza kusaini na kutangazwa rasmi na klabu yake hiyo tangu kufunguliwa kwa dirisha dogo la usajili lililoanza Desemba 16, mwaka huu.

## Timu za Ligi Kuu Bara zatikisa Kombe la FA

Na Adam Fungamwango

TIMU za Ligi Kuu zimeng'ara katika mechi za raundi ya pili ya Kombe la FA lililochezwa kwenye viwanja mbalimbali mwishoni mwa wiki kusaka bingwa atakayeiwakilisha nchi katika Kombe la Shirikisho barani Afrika msimu ujao.

Timu tano kati ya sita zilizocheza zimefanikiwa kwenda raundi ya tatu baada ya kupata ushindi katika mechi zao.

Timu hizo ni Singida Fountain Gate, Namungo FC, Geita Gold, Mashujaa FC na Tabora United, huku Prisons ikiangukia pua kwa kutolewa kwa mikwaju ya penalti.

Kwenye Uwanja wa Black Rhino Karatu, Arusha, timu ya Singida Fountain Gate, juzi iliishindilia Arusha City mabao 3-0, huku Namungo FC ikiachia kipigo cha mabao 5-0 dhidi ya Hollywood mechi iliyochezwa Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa, Lindi.

Geita Gold ilipata ushindi kama huo wa mabao 5-0 dhidi ya Singida Cluster, mechi ikipigwa Uwanja wa Nyankumbu, Geita na Uwanja wa Jamhuri Dodoma, ilishuhudiwa Tabora United ikiishindilia Mondoli Coffee mabao 4-1.

Mashujaa FC ikiwa Uwanja wa Lake Tanganyika, ilipata ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Mbuga.


Prisons pekee ndiyo ilishindwa kusonga mbele kwenye michuano hiyo juzi, ilipoondolewa kwa mikwaju ya penalti 6-5 dhidi ya TRA Kilimanjaro, mechi ikichezwa Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Timu hizo zililazimika kupigiana mikwaju ya penalti baada ya kumaliza dakika 90 bila kufungana.

Matokeo mengine ya raundi ya pili ya michuano hiyo, Ken-Gold ilikubali kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Gunners FC, Transit Camp ikaifunga Air Port mabao 2-1, na Cosmopolitan ikakubali kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Rhino Rangers.

**Prisons pekee ndiyo ilishindwa kusonga mbele kwenye michuano hiyo juzi, ilipoondolewa kwa mikwaju ya penalti 6-5 dhidi ya TRA Kilimanjaro, mechi ikichezwa Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.**

UMESTAHILI...




Meneja Masoko na Mawasiliano wa Lake Energies, Matina Nkurlu (kushoto), akikabidhi Tuzo ya Best Music Score, iliyoenda kwa Chumba Cheusi. Wakati wa Tuzo za Tanzania Film Award 2023, zilizofanyika juzi katika ukumbi wa The Super Dome, jijini Dar es Salaam na kudhaminiwa na Lake Energies. **MPIGAPICHA WETU**

## *Gamondi alia straika wakiisubiri Medeama*

INATOKA UKURASA 24

"Nafurahishwa na kiwango chake wakati tunaanza msimu nilimwambia anapaswa kuweka umakini kwenye uwanja wa mazoezi kwani anaweza kuwa mfungaji bora kwa kuwa ana ubora huo.

"Kwenye mchezo wa leo (juzi), angekaa kwenye maeneo sahihi angefunga mabao matatu au manne, nimefurahishwa na kiwango chake anajituma sana naamini ataendeleza zaidi ya hapo," alisema Gamondi.

Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, naye aliwapongeza wachezaji wake hasa kwa kipindi cha kwanza kucheza kwa nidhamu na kuweza kuwazuia Yanga, katika kutengeneza nafasi katikati kuanzia chini akisema ndio maana wakapata bao.

"Ukifanya makosa lazima utaadhibiwa ndio mpira ulivyo, lazima ukubali unacheza na timu ya aina gani na kama unafanya makosa ndio kama vile unaadhibiwa, lakini yote kwa yote tumecheza vizuri na tulitaka kushangaza watu, lakini ndio mpira.

Naishia hapa kusema tumefungwa, tunajipanga kwa mchezo ujao ambao uko karibu yetu, hakuna muda kesho (jana)tusafiri, tukajiweke sawa kucheza na Mashujaa," alisema Katwila.

## Benchikha aipa pumzi...

INATOKA UKURASA 24

Morocco dhidi ya UTS, ambayo Wydad Casablanca ilishinda bao 1-0.

Kajula alisema wanaimani kubwa na kocha wao kwa siku chache tangu alivyokabidhiwa kikosi kwani kuna mabadiliko makubwa yameonekana na siku za baadaye Simba itarejea katika ubora wake.

Katika hatua nyingine taarifa kutoka ndani ya Simba kuwa tayari wamekamilisha usajili wa wachezaji wapya watakaoingia katika dirisha dogo na baada ya mechi dhidi ya Wydad Casablanca, nyota hao wanatarajia kuanza kuwasili nchini muda wowote.

Mtoa habari huyo alisema Simba imepanga kufanya maboresho katika baadhi ya nafasi, baada ya Benchikha kukabidhi ripoti ya usajili ambayo inahitaji wachezaji zaidi katika usajili huu wa dirisha dogo.

"Tayari uongozi umemhakikishia fungu la fedha la kutosha litakalokamilisha usajili wa wachezaji, yeye mwenyewe amewapendekeza katika usajili huu uliofunguliwa Ijumaa iliyopita.

"Kocha ameachiwa jukumu lote la usajili, kwa wale wachezaji anaowataka ambao anaamini watakiboresha kikosi chake, kati ya hao wapo wa kigeni ambao baadhi alifanya nao kazi na klabu alizopita," alisema mtoa taarifa huyo.

# Michezo

Jumatatu Desemba 18, 2023

Nipashe




Xavi afadhaika kwa sare UKURASA 22



Aziz Ki

# Gamondi alia straika wakiisubiri Medeama

**Na Saada Akida**

## Ashangaa kupoteza nafasi 11, amtaja Aziz Ki huku akimtabiria kuwa...

LICHA ya ushindi mnono wa mabao 4-1 walioupata juzi dhidi ya Mtibwa Sugar, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, bado haridhishwi na ufanisi wa safu yake ya ushambuliaji wakati huu wakisubiri kuikaribisha Medeama ya Ghana kwenye mechi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

**Yanga itaikaribisha Medeama katika mchezo huo utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Jumatano wiki hii, ikisaka ushindi ili kurejesha matumaini ya kutinga robo fainali.**

Katika mechi ya juzi ya Ligi Kuu dhidi ya Mtibwa Sugar, pamoja na kuibuka na ushindi, lakini ilipoteza nafasi 11 za mabao, jambo ambalo Gamondi ameeleza kutoridhishwa na hali hiyo.

Ushindi huo umeifanya Yanga kuendelea kusalia kwenye nafasi ya pili ya msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 27 baada ya kushuka uwanjani mara 10 ikishinda michezo tisa na kupoteza mmoja.

Akizungumza baada ya dakika 90 kukamilika juzi, Gamondi alisema wachezaji licha ya kwamba haukuwa mchezo mgumu, lakini walikosa umakini kwa kushindwa kutumia nafasi walizotengeneza.

Alisema pamoja na kuwapongeza wachezaji wake kwa kuonesha mchezo mzuri, lakini bado ana kazi kubwa kwa watu wake hao ya kufunya kuhakikisha wanatumia nafasi wanazotengeneza kufunga magoli.

"Kipindi cha kwanza tulitengeneza nafasi za wazi 11, hilo ni tatizo tulipaswa kufunga mabao mengi, lakini baada ya mabao mawili mchezo ulibadilika tunatakiwa kuendelea kuboresha katika eneo hili kwenye mita 25.

"Unapotengeneza nafasi 11 unatakiwa kufunga zaidi, unajua unapocheza na timu aina ile unatakiwa kukaba, kufanya jitihada kubwa kuzuia. Kipindi cha pili tulikuwa tunaondoa mipira haraka na kutengeneza nafasi nyingi ambazo zilishindwa kugeuzwa kuwa mabao," alisema Gamondi.

Aliongeza kuwa amefurahishwa na kiwango kilichooneshwa na kiungo wake, Stephane Aziz Ki kwa kufikisha mabao tisa na kuwa kinara kwenye orodha ya wafungaji wa Ligi Kuu Bara kwa sasa.

INAENDELEA UKURASA 23

# Benchikha aipa pumzi Simba ushindi Wydad

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Klabu ya Simba umeangalia kundi lao la Ligi ya Mabingwa Afrika (CAFCL) na kudai wana kazi kubwa mbele yao wanayotakiwa kuifanya ya kuvuna pointi tatu kesho, Jumanne dhidi ya Wydad Casablanca ya Morocco, lakini wanaimani kubwa na Kocha Abdelhak Benchikha katika mbinu zake kuwapa ushindi.

Kikosi cha 'Wekundu wa Msimbazi' hao chini ya Kocha Benchikha, kinaendelea kujiandaa vizuri kuelekea mchezo wa marudiano dhidi ya Wydad utakaochezwa kesho katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam saa 10:00 jioni.

Akizungumza na Nipashe jana, Mtendaji Mkuu wa Simba, Imani Kajula, alisema msimu huu mashindano hayo yamekuwa na matokeo ya kustaajabisha kwa sababu ya timu kufanana pointi katika makundi mbalimbali.

Alisema katika kundi lao kila timu inaweza kwenda robo fainali kwa kila moja kushinda mechi alizonazo, hivyo bado nafasi kwao ipo lakini wako na kazi kubwa kwa wachezaji kupambana kutafuta matokeo katika mechi za marudiano.

"Hii ni mechi muhimu sana kwetu, kocha Benchikha anaendelea na maandalizi wachezaji wako kwenye morali nzuri, ushindi wetu dhidi ya Kagera Sugar umeongeza kitu, tunaimani kubwa kwa umoja na mshikamano wetu tunamfunga Wydad Casablanca hapa nyumbani.


"Haitakuwa mechi rahisi kwa sababu wapinzani wetu wamemwondoa kocha wao (Adil Ramzi), wanakuja kivingine kulingana na mabadiliko hayo tayari Benchikha amechukua tahadhari zote kuhakikisha tunashinda mechi dhidi ya Wydad," alisema Kajula.

Alieleza kuwa hawaidharau Wydad Casablanca na haitakuwa mechi rahisi kwa sababu ya wapinzani wao wanakumbukumbu ya kupoteza katika dimba la Benjamin Mkapa msimu uliopita katika mashindano hayo hatua ya robo fainali.

"Huu mchezo ni kutafuta ushindi, lakini pia kulipa kisasi, kocha wetu amefanyia kazi maeneo yenye mapungufu na kuongeza pale kwenye ubora, hasa eneo la mwisho kutumia nafasi na kufunga magoli, lakini pia safu ya ulinzi ," alisema mtendaji huyo.

Aliongeza kuwa hawana hofu juu ya mbinu kwa sababu Benchikha tayari anafanyia kazi ubora na udhaifu wa wapinzani wao baada ya kuwafuatilia juzi walipokuwa wakicheza mechi yao ya ligi ya nchini

INAENDELEA UKURASA 23



Abdelhak Benchikha

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >